NOVEMBA 11, 2026

/islamicftz

IMAAN

Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

ISSN 5618 - NO. 610



Pigo zito kwa Trump, Natanyahu

HISTORIA!

Masjid Al Ghaith waanza kutumika

- Aref Nahdi: Tuulinde uwekezaji huu
- Dar Al Ber yamwaga pongezi

Bismillah, Masjid Al Ghaith ni kielelezo cha usanifu wa kisasa wa Kiislamu kinachobeba uwezo wa waumini **3,000,** kikileta mwanga mpya wa **Ibada, Amani na Huduma kwa jamii nchini.**





Rais Samia atua nchini Uturuki, kuongoza ajenda ya nishati safi COP31

Wito: Taasisi ya Zaka duniani ifufuliwe



Dkt Mwinyi: Maendeleo bila amani? Haiwezekani!

Ajali iliyouwa 21 Iringa, Samia atuma salamu za pole »

Waziri wa Fedha mgeni rasmi kongamano la uwekezaji halali



Awqaaf Tanzania: Maeneo 4 muhimu kuwekeza Waqf

Samia atua Uturuki, kuongoza ajenda ya nishati safi COP31

Rais Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kutumia jukwaa la Mkutano wa 31 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP31), kuwasilisha vipaumbele vya Tanzania katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, huku akisisitiza upatikanaji wa fedha, teknolojia na utaalamu wa kuimarisha uwezo wa ndani.

Hatua hiyo inakuja wakati dunia ikielekeza nguvu katika utekelezaji wa makubaliano ya kimataifa badala ya kuendelea kutegemea ahadi na maazimio yasiyozaa matokeo yanayoonekana kwa wananchi.

Rais Samia aliondoka nchini jana kuelekea Antalya, Uturuki, kushiriki mkutano huo unaowakutanisha viongozi wa nchi mbalimbali kujadili hatua za pamoja za kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Bakari Machumu, Rais Samia anatarajiwa kuhutubia mkutano wa wakuu wa nchi na serikali, pamoja na kuongoza mjadala wa ngazi ya juu kuhusu kuharakisha matumizi ya nishati safi ya kupikia barani Afrika.

Pia anatarajiwa kufanya mazungumzo ya pande mbili na mwenyeji wake, Rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erdoğan, yakilenga juhudi za kupunguza uzalishaji wa gesi chafuzi na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mkutano huo ulioanza Novemba 9 unatarajiwa kuhitimishwa Novemba 20, 2026, ukiwa na ajenda zinazohusu fedha za tabianchi, nishati jadidifu, usalama wa chakula na miundombinu inayostahimili athari za hali mbaya ya hewa.

Akifungua mkutano huo, Katibu Mtendaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC), Simon Stiell, alizitaka nchi kuongeza kasi ya utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa katika mikutano iliyopita.

Alisema COP31 inapaswa kuwa mwanzo wa awamu mpya inayolenga kugeuza maazimio kuwa matokeo halisi, akibainisha kuwa hatua zilizopigwa bado hazijafikia kasi na kiwango cha usawa kinachohitajika.

Alitaja vipaumbele kuwa ni kuongeza fedha za kukabiliana na athari za tabianchi, kupanua matumizi ya nishati jadidifu, kuboresha miundombinu ya usafirishaji wa umeme na kupunguza uzalishaji wa gesi ya methane.

Katika eneo la ufadhili, Stiell alisisitiza umuhimu wa kuweka wazi namna ya kutekeleza ahadi ya dola bilioni 300 kila mwaka na kuhamasisha jumla ya dola trilioni 1.3 kwa ajili ya hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Tanzania yaweka vipaumbele

Akizungumza katika kikao cha maandalizi ya ujumbe wa Tanzania kilichofanyika Antalya Novemba 9, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Hamad Yussuf Masauni, alisema upatikanaji wa fedha na kujengewa uwezo kwa wataalamu wa ndani ni miongoni mwa vipaumbele vya nchi.

Alisema Tanzania inahitaji kutumia diplomasia ya tabianchi kuimarisha ushirikiano wa kimataifa, kupata teknolojia za kisasa na kuhakikisha ahadi za washirika wa maendeleo zinageuzwa kuwa msaada unaotekelezeka.

Masauni alisisitiza kuwa ujumbe wa Tanzania unapaswa kuwasilisha umuhimu wa matumizi endelevu ya rasilimali za taifa sambamba na kuomba ushirikiano wa kimataifa katika kukabiliana na changamoto za mazingira.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Richard Muyungi, alisema ujumbe wa Tanzania pia utakutana na wadau wa kimataifa kufuatilia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa kuhusu ufadhili wa tabianchi na mafunzo ya kitaalamu.

Ushiriki wa Tanzania katika COP31 unaongozwa na kaulimbiu: “Tanzania’s Inclusive Climate Action for Dira 2050: Building a Resilient, Green and Prosperous Nation.”

Naye Rais wa COP31 ambaye pia ni Waziri wa Mazingira, Miji na Mabadiliko ya Tabianchi wa Uturuki, Murat Kurum, alisema changamoto hiyo haihusu mazingira pekee, bali pia mifumo ya chakula, nishati, afya na maendeleo ya uchumi.



Rais Samia Suluhu Hassan, akiwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Antalya nchini Uturuki, tarehe 10 Novemba, 2026 kwa ajili ya kushiriki Mkutano wa 31 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabia (COP31).

Ijumaa ya kihistoria, Masjid Al Ghaith waanza kutumika

Zaidi ya waumini 8,000 waswali ijumaa ya kwanza

Msikiti mpya wa Al Ghaith utajikita katika misingi mitatu ya kufundisha Akida sahihi, kufuata Sunnah za Mtume Muhammad (SAW) na kuimarisha malezi ya Kiislamu kwa watoto, vijana na wazee.

Hayo yameelezwa na mlinganiaji wa Kiislamu, Sheikh Ibrahim Twaha, wakati wa Swala ya kwanza ya Ijumaa iliyoswaliwa katika msikiti huo, baada ya kukamilika kwa ujenzi wake uliosimamiwa na taasisi ya The Islamic Foundation.

"Msikiti huu tuhakikishe tunautumia kwa manufaa. Tutahakikisha Msikiti wa Al Ghaith unasimama kwa misingi mitatu ambayo ni Akida sahihi, kufuata Sunnah na kuongoza malezi," amesema Sheikh Twaha.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa The Islamic Foundation, Aref Nahdi, amewataka Waislamu na jamii kwa ujumla kuulinda na kuutunza msikiti huo ili uweze kuendelea kutoa manufaa kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

"Tunawasihi Waislamu wote na jamii kwa ujumla kudumisha na kulinda uwekezaji huu mkubwa wa nyumba ya ibada. Tunaamini utakuwa na manufaa makubwa mno kwa kizazi hiki na hata kingine ikiwa tutashikamana pamoja," amesema Nahdi.

Mtoto wa mhisani ashuhudia Swala ya kwanza

Ibada hiyo ya kihistoria ilihudhuriwa na Abuu Muhammad, mtoto wa mhisani mkuu, Sheikh Muhammad Said Al Ghaith, aliyefadhili ujenzi wa msikiti huo kwa ajili ya kuwahudumia waumini na jamii ya Kiislamu.

Abuu Muhammad aliambatana na Mkurugenzi wa taasisi ya Dar Al Ber, Imran Mohammad, ambaye pia alishiriki Swala hiyo ya kwanza ya Ijumaa.

Sheikh Twaha alitumia fursa hiyo kumwombea dua mhisani Sheikh Muhammad Said Al Ghaith kwa kutenga mali yake kufanikisha ujenzi wa msikiti huo.

"Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu amlipe kila lililo la kheri na ampe umri mrefu na afya njema mhisani mkuu Muhammad Said Al Ghaith kwa kutenga mali yake kwa ajili ya msikiti huu," amesema.

Dar Al Ber yaipongeza ujenzi

Mkurugenzi wa Dar Al Ber, Imran Mohammad, ameipongeza The Islamic Foundation kwa usimamizi wa ujenzi wa msikiti huo na kuwataka waumini kuendelea kushiriki katika ibada na matendo mema.

Alisisitiza kuwa kujitolea kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya ibada ni amali yenye uzito mkubwa mbele ya Mwenyezi Mungu.

"Mwenyezi Mungu azijaalie amali hizi za kujitolea kuwa na uzito mkubwa, na ziwe na uzito kwa kila aliyeshiriki nasi kwa ajili ya msikiti huu," amesema Imran.

Baada ya Swala, Imran na wageni alioambatana nao walitembezwa na kukagua maeneo mbalimbali ya msikiti huo ili kujionea ubora wa ujenzi, mpangilio wa jengo na miundombinu iliyowekwa kwa ajili ya kurahisisha ibada na kuwahudumia waumini.

Ziara hiyo iliwapa wageni fursa ya kufahamu hatua mbalimbali za utekelezaji wa mradi huo na jitihada za The Islamic Foundation katika kuhakikisha ujenzi unakamilika kwa viwango vilivyokusudiwa.

Waumini wafurahia kuanza kutumika kwa msikiti

Waumini waliohudhuria Swala hiyo ya kwanza wameeleza furaha yao na kuipongeza The Islamic Foundation kwa usimamizi wa mradi huo tangu kuanza kwa ujenzi hadi kukamilika kwake.

Mmoja wa waumini hao, Omar Rashid, amesema uongozi wa taasisi hiyo umeonyesha usimamizi mzuri uliowezesha kukamilika kwa msikiti wenye viwango vya juu.

"Tunajivunia sana jitihada za viongozi wa The Islamic Foundation kwa usimamizi mzuri tangu kuanza kwa mradi wa ujenzi hadi kukamilika kwake. Usimamizi ulioleta matunda bora ya nyumba hii ya viwango vya juu ya kufanyia ibada," amesema Omar.

Naye Mansour Haroon alisema Waumini walikuwa wameisubiri kwa hamu siku ya kuanza kuswali katika msikiti huo.

"Tumesubiri kwa hamu kubwa sana siku hii. Hatimaye imekuwa. Nimefurahi sana kuona tunaswali hapa kwa pamoja kwa mara ya kwanza. Hii ni faraja na neema kubwa sana kwetu," amesema Mansour.

Aliwaombea kheri wote walioshiriki katika ujenzi wa msikiti huo.

Kukamilika kwa msikiti huo kunatarajiwa kufungua fursa mpya za kuimarisha maisha ya kiimani, kimaadili na kijamii kupitia ibada za kila siku, mafundisho ya dini na shughuli mbalimbali za malezi kwa watoto, vijana na jamii kwa ujumla.




٣٠
جُمَادَى الأُولَى
١٤٤٨ هـ



MATUKIO KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar
0655 763 580

Ijumaa ya kihistoria, Masjid Al Ghaith waanza kutumika















Ajali yauwa 21, Samia atuma salamu zapole

Wanaume 10, wanawake tisa na watoto wawili miongoni mwa waliofariki dunia, huku wengine watano wakijeruhiwa

WATU 21 wamefariki dunia na wengine watano kujeruhiwa baada ya basi la abiria kugongana na lori la mizigo katika ajali iliyotokea kwenye Barabara Kuu ya Iringa–Mbeya, mkoani Iringa, huku Rais Samia Suluhu Hassan akituma salamu za rambirambi kwa familia zilizopoteza wapendwa wao.

Ajali hiyo iliyotokea asubuhi ya Novemba 8, 2026, katika eneo la Njiapanda ya Kiponzero, imesababisha vifo vya wanaume 10, wanawake tisa na watoto wawili, kwa mujibu wa taarifa ya Jeshi la Polisi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, ACP Allan Bukumbi, amesema basi lililokuwa likifanya safari zake kutoka Iringa Mjini kuelekea Kiponzero linadaiwa kufeli breki wakati likitokea kwenye barabara ya vumbi na kuingia Barabara Kuu.

Amesema tukio hilo limesababisha vifo vya watu 21, huku wengine watano wakijeruhiwa na kuhitaji matibabu.

Idadi hiyo ya vifo imeifanya ajali hiyo kuwa miongoni mwa matukio yenye maafa makubwa, ikigusa familia nyingi zilizopoteza ndugu na jamaa zao, wakiwemo watoto wawili.

Samia atuma rambirambi

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameeleza kusikitishwa na vifo vya watu hao, akituma salamu za rambirambi kwa viongozi wa mkoa na familia zilizokumbwa na msiba huo.

Kupitia ujumbe wake, Rais Samia amesema amepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za ajali hiyo iliyohusisha basi la abiria na lori la mizigo katika eneo la Masumbo, kwenye Barabara ya Iringa–Mbeya, mkoani Iringa.

Ametoa pole kwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Kheri James, familia, ndugu na jamaa wa marehemu, pamoja na Watanzania wote waliloguswa na tukio hilo.

Aidha, amewaombea wafiwa wapate faraja, subira na nguvu ya kukabiliana na kipindi hicho kigumu cha maombolezo, huku akiwaombea majeruhi watano wapone haraka na kurejea katika hali zao za kawaida.

“Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema, amina,” amesema Rais Samia.

Usalama barabarani

Ajali hiyo imeendelea kuibua umuhimu wa ukaguzi wa mara kwa mara wa vyombo vya usafiri, hususan mifumo ya breki, ili kuhakikisha magari yanayobeba abiria yanakuwa katika hali salama kabla ya kuanza safari.

Pia, inasisitiza wajibu wa madereva kuhakikisha wanazingatia tahadhari zote za usalama barabarani, kwa kuwa hitilafu za kiufundi zinaweza kusababisha madhara makubwa kwa abiria na watumiaji wengine wa barabara.

Mwinyi: Maendeleo bila amani? Haiwezekani!



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amewataka wananchi kuendelea kulinda amani na utulivu, akisema hali hiyo ni nguzo muhimu ya maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii.

Amesema mazingira ya amani na utulivu yana nafasi kubwa katika kuvutia wawekezaji, kukuza biashara na kuimarisha sekta ya utalii, hivyo ni wajibu wa kila mwananchi kushiriki katika kuyadumisha.

Dkt. Mwinyi aliyasema hayo Novemba 9, 2026, wakati wa Dua Maalumu ya Kitaifa ya kuiombea Zanzibar na Tanzania kwa ujumla amani na ulinzi dhidi ya majanga mbalimbali, iliyofanyika katika Msikiti wa Muembe Shauri, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisisitiza kuwa amani si jukumu la Serikali pekee, bali ni wajibu wa wananchi wote, wakiwemo viongozi wa dini, kuilinda kwa vitendo kupitia kuhimiza umoja, mshikamano, upendo na kuheshimiana.

Alisema viongozi wa dini wana nafasi muhimu katika kujenga jamii yenye maadili mema na kuzuia vitendo vinavyoweza kuvuruga mshikamano wa wananchi.

Aidha, Rais Mwinyi alitumia fursa hiyo kuwaasa wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya athari zinazoweza kusababishwa na mvua za Vuli na El Niño, akihimiza kuzingatia maelekezo ya mamlaka husika ili kujikinga na majanga yanayoweza kujitokeza.

Dua hiyo iliyoandaliwa na Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar ililenga kuiombea nchi amani, usalama na kinga dhidi ya majanga mbalimbali yanayoweza kuathiri maisha ya wananchi.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali na dini, akiwemo Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, pamoja na Rais Mstaafu wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohamed Shein.

Ujumbe wa Rais Mwinyi umeweka msisitizo katika umuhimu wa kulinda amani kama msingi wa kuendeleza shughuli za kiuchumi, kuvutia mitaji na kuhakikisha wananchi wanaendelea kuishi katika mazingira salama na yenye utulivu.

Waziri wa Fedha mgeni rasmi kongamano la uwekezaji halali

■ Ni Alhamisi hii Nov 12 ■ Wataalamu benki, Sharia na masoko ya mitaji kushiriki ■ Kampuni changa kuwasilisha miradi mbele ya wawekezaji

WAZIRI wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika Kongamano la Uwekezaji Halali Tanzania, litakalowakutanisha wawekezaji, wataalamu na viongozi wa taasisi za fedha kujadili upatikanaji wa mitaji inayozingatia Sharia na mchango wake katika maendeleo ya taifa.

Kwa mujibu wa tangazo jipya la waandaaji, kongamano hilo, Tanzania Halal Investment Summit 2026, litafanyika Novemba 12 katika Hoteli ya Hyatt Regency, Dar es Salaam, kuanzia saa 2:30 asubuhi hadi saa 10 jioni.

Kongamano linaandaliwa na Shirkah kwa kushirikiana na Kituo cha Fedha za Kiislamu, Uzingatiaji na Ushauri (CIFCA) pamoja na Taqseem Academy, likiwa na kaulimbiu "Halal Investing Towards a US$1 Trillion Economy".

Ushiriki uliotangazwa wa Waziri wa Fedha unakuja wakati waandaaji wakilenga kuibua mjadala kuhusu namna uwekezaji unaozingatia Sharia unavyoweza kusaidia kugharamia biashara na miradi ya maendeleo kuelekea malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Akizungumza awali na Gazeti IMAAN, Salum Awadh, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirkah Asset Management, alisema waandaaji wanataka kuimarisha uelewa wa fursa za uwekezaji halali na mazingira yanayohitajika kuziendeleza.

"Tunataka Waziri wa Fedha aondoke na mtazamo kwamba huduma za fedha za Kiislamu zina mchango mkubwa katika Dira 2050, hivyo Serikali iweke mazingira sahihi ya kutumia huduma hizi kwa ajili ya miradi mikubwa ya Serikali," alisema.


Wataalamu kushiriki

Kwa mujibu wa Hassan Rajab, mmoja wa waratibu wa kongamano, wazungumzaji watakuwa Awadh; Sheikh Mohamed Issa, Mwenyekiti wa Yusra Sukuk na mhamasishaji wa uwekezaji kupitia sukuk; pamoja na Sheikh Muharram Mwaita, mwanazuoni na Mkurugenzi wa Africa TV.

Sukuk ni hati za uwekezaji zinazoundwa kwa kuzingatia misingi ya Sharia.

Washiriki wa mijadala watakuwa Dkt. Huda Yussuf, mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA); Amour Muro, Mkuu wa Huduma za Benki za Kiislamu wa KCB Bank Tanzania; na Ramadhan Kagwandi, Mkurugenzi Mtendaji wa Exodus Advisory Services.

Wengine ni Aisha Mbilizi kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA); Rashid H. Rashid, Mkuu wa CRDB Albarakah Banking; Yassir Masoud kutoka Umoja wa Wanazuoni Tanzania, Hay-atul Ulamaa; na Salim Bharwani, mshirika katika Twelfth Law & Advisory.



Pia watashiriki Khalfan Abdallah, Mkuu wa Bidhaa na Uzingatiaji wa Sharia katika SIB Najah; Gerase Kamugisha kutoka Alpha Capital; na Rajab Ramia kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

Mijadala itahusu fursa za uwekezaji unaozingatia Sharia, upatikanaji wa mitaji kwa biashara ndogo na za kati, uchunguzi wa uhalali wa uwekezaji na mazingira ya kisera na kisheria ya kuendeleza sekta hiyo.

Kampuni changa kutafuta mitaji

Rajab amesema kongamano litakuwa pia na kipindi cha wajasiriamali kuwasilisha miradi yao mbele ya wawekezaji, huku Jumanne Mtambalike, Mkurugenzi Mtendaji wa Sahara Ventures, akiwa jaji mkuu.

Katika maelezo yaliyotolewa awali, Muandaaji wa tukio hilo na wa Shirkah, Salum Awadh, alisema nafasi zimetengwa kwa kampuni changa tano, kila moja ikipewa dakika saba kuwasilisha mradi na dakika tano kujibu maswali.

Kipengele hicho kinalenga kuwapa wajasiriamali nafasi ya kutafuta mitaji na kujenga mahusiano na wawekezaji wanaotafuta biashara zinazokidhi masharti ya uwekezaji halali.

Miongoni mwa wengine wanaotarajiwa kuhudhuria ni Prof. Mohammed Hafidh Khalfan, Mwenyekiti wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar na Makamu Mwenyekiti wa CIFCA; pamoja na Dkt. Muhsin Masoud, mwanabenki na mwanazuoni aliyewahi kuongoza Amana Bank na PBZ.

Pia anatarajiwa kuwapo Mkurugenzi Mtendaji wa PBZ, CPA Fahad Soud Hamid kwa mujibu wa taarifa katika mitandao ya kijamii ya Shirkah Invest.

Kongamano linalenga wawekezaji binafsi, taasisi za fedha, wajasiriamali, watunga sera, wataalamu wa Sharia na wanafunzi wa taaluma za fedha. Kwa mujibu wa tangazo jipya, tiketi zinapatikana kupitia www.tikeza.co.tz.

CIFCA, ZIAAT zaanza utekelezaji MOU

Ni makubaliano yanalenga kuboresha huduma fedha za Kiislamu Zanzibar

Kituo cha Uzingatiaji wa Sharia na Ushauri wa Fedha za Kiislamu (CIFCA) na Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri wa Kodi Zanzibar (ZIAAT) zimeunda kamati za watu watatu kila upande kuratibu utekelezaji wa makubaliano ya miaka minne ya kujenga uwezo wa wataalamu, yaliyosainiwa wiki iliyopita.

Kamati ya ZIAAT inajumuisha Khamis M. Khamis, Faki M. Faki na Salum Kh. Rashid, huku waliopendekezwa upande wa CIFCA wakiwa Katibu Mkuu wa taasisi hiyo, Salum Shaban Lupande, Jumanne Bundala na Juma Issa huku kikao cha kwanza cha kamati kikitarajiwa kufanyika Novemba 24, 2026.

MOU kati ya taasisi hizo mbili yaliyosainiwa Oktoba 28, 2026, na Makamu Mwenyekiti wa CIFCA, Prof. Mohammed Hafidh, na Mkurugenzi Mtendaji wa ZIAAT, CPA Ame B. Shadhil, yalilenga kuimarisha taaluma katika huduma za fedha zinazozingatia Sharia, uhasibu, ukaguzi, kodi, usimamizi wa vihatarishi na uandaaji wa taarifa za fedha.

Akizungumza katika hafla hiyo, Prof. Hafidh alisema maendeleo ya sekta yanahitaji wahasibu wanaoelewa miamala, wakaguzi wanaoweza kutathmini ushahidi na wasimamizi wenye uwezo wa kubaini mapungufu na kuhakikisha yanarekebishwa.

Alisema utaalamu huo ni muhimu kujenga imani ya wananchi na wawekezaji kwamba huduma zinazotangazwa kuwa za Kiislamu zinaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya Sharia.

Prof. Hafidh alieleza kuwa makubaliano hayo yanarasimisha ushirikiano uliokwishaanza kati ya taasisi hizo. “Safari ilishaanza,” alisema, akisisitiza umuhimu wa kuhakikisha ushirikiano huo unazalisha matokeo yanayoonekana.

Aliipongeza ZIAAT kwa juhudi za kuwajengea uwezo wanachama wake, huku akiwasilisha salamu za Mwenyekiti wa CIFCA, Sheikh Aref Nahdi.

Kwa upande wake, CPA Ame Shadhil alisema ushirikiano huo utawezesha mafunzo, kubadilishana maarifa na kushirikiana katika tafiti.

Zanzibar kuelekea viwango vya kimataifa

Sehemu muhimu ya makubaliano ni maandalizi ya matumizi ya viwango vya kimataifa vya fedha za Kiislamu vinavyoandaliwa na Shirika la Uhasibu na Ukaguzi wa Taasisi za Fedha za Kiislamu (AAOIFI), lenye makao makuu Bahrain.

Katibu Mkuu wa CIFCA, Salum Lupande, alisema ZIAAT tayari imewasilisha maombi rasmi ya uanachama wa AAOIFI, huku CIFCA ikiendelea kusaidia mawasiliano na maandalizi ya mafunzo kuhusu viwango hivyo.

Juhudi hizo zilianza mwaka 2024 na kuendelezwa kupitia mazungumzo yaliyofanyika Bahrain, Aprili 2025. CIFCA ilisaidia ZIAAT kuandaa maombi ya kujenga uwezo na kushirikisha mamlaka za Serikali.

Prof. Hafidh alisisitiza kuwa matumizi rasmi ya viwango hivyo yatahitaji ushirikishwaji wa mamlaka husika na kufuata taratibu za kisheria.

Mafunzo Tanzania Bara na Zanzibar

Makubaliano yanahusisha programu mbili za pamoja kila mwaka, moja Zanzibar na nyingine Tanzania Bara, zikiwemo semina, warsha, kozi fupi na mafunzo endelevu ya kitaaluma.

CIFCA itatumia uzoefu wake na mitandao ya kimataifa kusaidia upatikanaji wa wakufunzi, nyenzo na maarifa mapya. Pia ina uzoefu wa kuratibu mafunzo na mitihani ya AAOIFI nchini Tanzania.

Timu ya pamoja itaundwa kuratibu utekelezaji, kubaini mahitaji ya mafunzo na kutoa taarifa za maendeleo kila baada ya miezi mitatu.

Prof. Hafidh alisisitiza umuhimu wa kupima mafanikio kwa shughuli zilizotekelezwa, watu walionufaika na matumizi halisi ya maarifa yaliyopatikana.

Aidha, alihimiza waajiri na taasisi za fedha kusaidia wataalamu kushiriki mafunzo, huku akisisitiza uwazi wa bajeti na uwajibikaji.

Ushirikiano huo unatarajiwa kujenga wataalamu wenye uwezo wa kutumia viwango vya kimataifa na kuendeleza maarifa ndani ya taa-





Rais Samia avutia Tanzania mitaji ya Qatar

Kampuni ya Thirty-Five Investment Holding yaonesha nia ya kuwekeza Kongwa, Dodoma na Bandari ya Uvuvi Kilwa, pia yachunguza miundombinu ya usafiri Zanzibar

KAMPUNI ya Thirty-Five Investment Holding ya Qatar imeonesha nia ya kuwekeza katika sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi na usafiri nchini, katika hatua inayoweza kufungua fursa mpya za mitaji, uzalishaji na ajira.

Nia hiyo imewasilishwa na Mwenyekiti wa kampuni hiyo, Dkt. Khalid bin Mohammed bin Abdullah Al Attiyah, katika mazungumzo na Rais Samia Suluhu Hassan yaliyofanyika Novemba 6, 2026, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotiwa saini na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Bakari Machumu, mazungumzo hayo yalijikita katika maeneo yenye fursa za uwekezaji, yakiwemo uzalishaji wa sukari, ufugaji wa ng'ombe, uvuvi wa bahari kuu na miundombinu ya usafiri.

Katika sekta ya kilimo na mifugo, kampuni hiyo imeonesha nia ya kuwekeza katika uzalishaji wa sukari na ufugaji wa ng'ombe katika eneo la Kongwa, mkoani Dodoma.

Miradi hiyo inaibua fursa za kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo, kupanua shughuli za kiuchumi na kuchochea uwekezaji katika maeneo ya uzalishaji.

Uwekezaji bandari ya kilwa

Katika sekta ya uvuvi, majadiliano yalihusu uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu, ujenzi wa mitambo ya kuchakata samaki pamoja na miundombinu ya kuhifadhi mazao ya uvuvi katika Bandari ya Uvuvi Kilwa.

Uwekezaji unaopendekezwa unalenga kuimarisha mnyororo mzima wa thamani katika sekta hiyo, kuanzia upatikanaji wa samaki baharini hadi uchakataji, uhifadhi na maandalizi ya bidhaa kwa ajili ya masoko.

Kuwepo kwa mitambo ya kisasa ya kuchakata samaki na miundombinu bora ya uhifadhi kunatarajiwa kuongeza uwezo wa kuongeza thamani ya mazao ya baharini, kupunguza upotevu wa bidhaa zinazoharibika na kupanua shughuli za kiuchumi zinazotokana na uvuvi.

Kwa upande wa Zanzibar, Dkt. Al Attiyah alisema kampuni yake inatathmini fursa za uwekezaji katika miundombinu ya usafiri, huku mazungumzo ya awali yakiwa yameanza na wataalamu kutoka taasisi husika.

Hatua hiyo inaonesha wigo wa mazungumzo ya uwekezaji kuvuka sekta za uzalishaji na kujumuisha miundombinu inayoweza kusaidia kurahisisha usafirishaji wa watu na bidhaa.

Samia atoa maelekezo

Akizungumzia hatua inayopaswa kufuatia mazungumzo hayo, Rais Samia amezitaka taasisi za Serikali kuendeleza majadiliano na kampuni hiyo kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni za nchi.

Amesisitiza umuhimu wa kuchambua mapendekezo hayo ili kubaini miradi inayotekelezeka, yenye tija na manufaa kwa pande zote.

Maelekezo hayo yanaweka msisitizo katika kuhakikisha nia ya uwekezaji inageuzwa kuwa miradi inayoweza kutekelezwa kwa kuzingatia maslahi ya taifa na mazingira ya biashara nchini.

Iwapo mapendekezo hayo yatafikia hatua ya utekelezaji, uwekezaji katika maeneo yaliyotajwa unaweza kuongeza shughuli za uzalishaji, kuchochea uchakataji wa bidhaa ndani ya nchi na kufungua fursa zaidi katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na usafiri.

IMAAN

UCHAMBUZI WA KIUCHUMI



SHEIKH
Mohamed Issa
0762 715 311

Ushoroba wa Lobito waongeza ushindani kwa Tanzania

■ Njia ya biashara kupitia Angola yaweza kupunguza mizigo na mapato ya usafirishaji ■ Tanzania inahitaji kuimarisha reli, barabara na huduma za bandari

Tanzania inakabiliwa na ushindani unaoongezeka katika biashara ya kusafirisha mizigo ya Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), wakati Ushoroba wa Lobito, unaopita Angola, ukiimarishwa.

Njia hiyo ya kuelekea Bahari ya Atlantiki inaweza kuvutia sehemu ya mizigo inayopitia Bandari ya Dar es Salaam na kupunguza mapato ya kampuni za usafirishaji, maghala na huduma nyingine.

Hata hivyo, si ushahidi wa mgogoro wa kiuchumi unaokaribia. Ni tahadhari kwamba Tanzania inahitaji kupunguza gharama na kuongeza uhakika wa huduma kabla wateja hawajachagua njia nyingine.

Ushoroba wa Lobito umefikia wapi?

Reli iliyopo inaunganisha Bandari ya Lobito nchini Angola na maeneo ya madini kusini mwa DRC. Kiungo kipya kinachopangwa kuelekea Zambia kinatarajiwa kuongeza ushindani katika usafirishaji wa mizigo ya ukanda wa shaba.

Kampuni ya Lobito Atlantic Railway iliripoti kusafirisha karibu tani 200,000 za mizigo ya kimataifa mwaka 2025. Huo ni utendaji wa reli inayofanya kazi sasa, si wa kiungo kipya cha Zambia.

Kwa mujibu wa Africa Finance Corporation (AFC), reli mpya ya takribani kilomita 830 itaunganisha Chingola, Zambia, na Luacano, Angola. AFC inalenga kukamilisha taratibu za ufadhili mwaka 2027.

Lengo la tani milioni tano kwa mwaka ni matarajio ya baadaye, si mizigo inayosafirishwa leo. Ufadhili wa 2027 haupaswi kuchanganywa na tarehe ya kukamilika kwa ujenzi.

Kwa nini Tanzania inapaswa kujali?

Takwimu za Bandari ya Dar es Salaam zinaonyesha ukubwa wa biashara inayoshindaniwa. Kwa mujibu wa taarifa ya The Citizen iliyomnukuu mkurugenzi wa bandari, mizigo ya DRC ilikuwa tani milioni 7.77 na ya Zambia tani milioni 3.41 katika mwaka wa fedha 2025/26.

Tani hizo milioni 11.18 zilikuwa asilimia 76.5 ya tani milioni 14.61 za mizigo ya kupita nchini na asilimia 33.2 ya tani milioni 33.71 za mizigo yote iliyohudumiwa bandarini.

Hata hivyo, si mizigo yote inaweza kuhamia Lobito. Maeneo tofauti ya DRC hutumia njia tofauti, na Lobito pia inaweza kuvutia mizigo kutoka bandari nyingine za kusini mwa Afrika au kutokana na ukuaji wa biashara.

Athari zinazoweza kutokea

Ikiwa mizigo itapungua, athari zitavuka mipaka ya bandari. Waendeshaji wa malori na reli, maghala, kampuni za uondoshaji mizigo, madereva na biashara za kando ya barabara wanaweza kupoteza mapato na ajira.

Benki zinazofadhili malori na maghala nazo zinaweza kuathirika ikiwa wakopaji watashindwa kulipa.

Hata hivyo, thamani ya madini yanayopita Tanzania si mapato yote ya Tanzania. Kinachoweza kupotea ni mapato na thamani inayoongezwa kupitia huduma za usafirishaji, pamoja na kodi na ada zinazokusanywa.

Mizigo ya kupita nchini haipaswi kuhesabiwa kama bidhaa zote zinazotozwa kodi ya kuingiza nchini.

Kwa mfano, asilimia 20 ya mizigo hiyo ya Zambia na DRC ikihamia njia nyingine, upungufu ungekuwa tani milioni 2.24, sawa na asilimia 6.6 ya mizigo yote iliyohudumiwa bandarini mwaka 2025/26. Huu ni mfano wa kihesabu, si utabiri.

Hatari ya muda mrefu ni Tanzania kuendelea kuongeza mizigo, lakini ikapata sehemu ndogo ya ukuaji wa biashara ya kikanda kuliko ingeweza kupata.

Tanzania ifanye nini?

Kipaumbele ni kuboresha safari nzima ya mzigo, kutoka bandarini hadi kwa mteja. Huduma ya haraka bandarini haina maana kubwa ikiwa mzigo unachelewa kwenye reli, barabara au mpaka.

Kwanza, Tanzania iendeleze ufufuaji wa TAZARA. Taarifa ya TAZARA ya Oktoba 2026 inaonyesha makubaliano ya uwekezaji wa dola za Marekani bilioni 1.4 na kampuni ya CCECC kwa miundombinu na vifaa.

Makubaliano hayo bado yana masharti yanayopaswa kutimizwa kabla ya kuanza kutumika kikamilifu. TAZARA inalenga kusafirisha tani milioni 1.2 kwa mwaka 2029/30 na milioni 1.8 mwaka 2030/31, kutegemea utekelezaji.

Pili, barabara ya Dar es Salaam–Tunduma ipanuliwe kwa awamu kuelekea njia nne za magari, mbili kila upande, kuanzia maeneo yenye msongamano na hatari.

Ucheleweshaji mipakani na kwenye mizani upunguzwe kupitia ukaguzi ulioratibiwa na teknolojia ya kupima uzito magari yakiwa yanatembea, bila kulegeza usalama.

Tatu, vituo vya mizigo vya Kwala na Isaka viunganishwe na huduma za reli, barabara na forodha zenye uhakika. Kwala inaweza kurahisisha mizigo inayopitia Dar es Salaam, huku Isaka ikihudumia masoko ya bara.

Serikali na sekta binafsi zitafute mikataba ya muda mrefu ya mizigo na kuendeleza shughuli za usambazaji, uchakataji na matengenezo. Ufadhili wa uwekezaji mpya, ikiwemo ubia na Sukuk, uzingatie ushindani na mapato halisi yanayotarajiwa.

Tanzania ina faida ya kuwa lango la Bahari ya Hindi kwa biashara na Asia, lakini jiografia pekee haitoshi. Wateja watapima gharama, muda na uhakika wa kufikisha mizigo.

Lobito si mwisho wa nafasi ya Dar es Salaam. Kipindi ambacho reli mpya ya Zambia bado inaandaliwa ni fursa ya kuimarisha ushindani.

Nchi itakayotoa huduma za uhakika kwa bei shindani ndiyo itakayovutia mizigo ya kesho.

٣٠
جُمَادَى الأُولَى
١٤٤٨ هـ

CRDB mshirika uazishwaji kituo cha ubunifu Dubai



BENKI ya CRDB imetajwa kuwa mmoja wa washirika wanne katika mpango wa kuanzisha Kituo cha Ubunifu wa Fedha za Kiislamu Dubai, kitakachosaidia kuendeleza huduma zinazofuata Sharia kupitia ushirikiano wa kimataifa.

Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Falme za Kiarabu (WAM), DIFC Innovation Hub ilitangaza mpango huo Novemba 4 katika Jukwaa la Mustakabali wa Fedha za Kiislamu, sehemu ya Dubai Future Finance Week iliyofanyika Novemba 2–6, 2026.

Jukwaa hilo lilikutanisha washiriki zaidi ya 1,000 kutoka nchi zaidi ya 50 kujadili upatikanaji wa ukwasi baina ya masoko, uratibu wa kanuni na uwekezaji unaozingatia misingi ya Kiislamu.

Washirika wengine ni Emirates Islamic Bank, Principle Investor Group na Standard Chartered Saadiq. CRDB imesema ndiyo taasisi pekee kutoka Afrika katika kundi hilo, ikiwakilishwa na Mkuu wa Albarakah Banking, Rashid Rashid.

WAM inaeleza kuwa kituo kitaongozwa na DIFC Innovation Hub, kikiunganisha taasisi za fedha, wasimamizi, wanazuoni wa Sharia, watunga viwango na kampuni za teknolojia kutatua changamoto za pamoja.

Ushirikiano huo utasaidia kutambua mahitaji yanayofanana, kujaribu suluhisho na kuharakisha matumizi yake katika masoko mbalimbali, huku ukiimarisha miunganisho ya kifedha kati ya nchi zinazoendelea.

Kwa mujibu wa CRDB, ofisi yake ya uwakilishi Dubai ni daraja la kuimarisha mahusiano na taasisi za kimataifa, kutambua fursa za uwekezaji na kuiunganisha benki na mifumo ya ubunifu wa kifedha.

Katika taarifa yake katika mitandao ya kijamii, nukuu moja inasema: “Benki ya CRDB kuwa mshirika mwanzilishi wa kituo hiki cha ubunifu ni uthibitisho wa uongozi mahiri na dhamira yake ya kuendeleza ubunifu katika sekta ya fedha, sambamba na kupanua wigo wa ujumuishaji wa huduma za fedha kupitia huduma zake za kibenki za Kiislamu.”

Benki inasema ushiriki wake utatoa nafasi ya kubadilishana maarifa na uzoefu wa kimataifa, pamoja na kushiriki kuendeleza huduma zinazofuata Sharia na kukidhi mahitaji ya wateja.

Kupitia Albarakah Banking, CRDB inalenga kutumia ushirikiano huo kupanua ujumuishaji wa kifedha, huku ikipata fursa ya kuchangia mwelekeo wa maendeleo ya sekta hiyo.

زكاة

NA
Baitulmaal Tanzania

JUKWAA LA ZAKA

Historia ya usimamizi wa Zaka na maendeleo ya Baytulmaal

Usimamizi wa Zaka wakati wa Mtume Muhammad

Katika kipindi cha Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani), Zaka ilitekelezwa kama sehemu ya mfumo wa ibada na wajibu wa kijamii wa Waislamu. Mtume alielekeza ukusanyaji wake, akateua watu kwa kazi maalumu na kuhakikisha mali zilizokusanywa zinapelekwa kwa wanaostahiki.

Mtume alituma maafisa kwenda kwa jamii mbalimbali kukusanya Zaka. Hili lilikuwa jukumu la kiutawala lililohitaji uaminifu, elimu ya hukumu za Zaka na uadilifu.

Mfano unaojulikana ni Muadh ibn Jabal (Allah amridhie), ambaye Mtume alimtuma Yemen na kumwelekeza awafundishe watu wajibu wa Zaka, kwamba ichukuliwe kutoka kwa matajiri wao na kurudishwa kwa maskini wao. [Sahih al-Bukhari, 1395; Sahih Muslim, 19].

Mfano huu unaonyesha kuwa ukusanyaji wa Zaka haukuwa tu suala la mtu tajiri kuamua kumpa mtu yeyote, bali kulikuwa na utaratibu wa kuhakikisha haki ya wahitaji inafikiwa.

Mtume pia alisisitiza uadilifu katika ukusanyaji wa Zaka. Maafisa hawakupaswa kuwadhulumu watu, kuchukua mali isiyostahiki kuchukuliwa au kujinufaisha kupitia nafasi zao.

Katika Hadith ya Ibn al-Lutbiyyah, aliyeteuliwa kukusanya Zaka, Mtume alikemea tabia ya afisa kudai kwamba sehemu ya mali aliyoileta ilikuwa zawadi aliyopewa binafsi. [Sahih al-Bukhari, 7174; Sahih Muslim, 1832].

Tukio hili linafundisha umuhimu wa uwajibikaji wa maafisa, kuzuia matumizi mabaya ya mamlaka, kutenganisha mali ya umma na manufaa binafsi, uwazi kuhusu mali inayokusanywa na uadilifu kwa walipaji na walengwa.

Hizi ni kanuni ambazo taasisi ya Baytulmaal Tanzania inajifunza na kuzitekeleza kupitia mifumo ya kisasa ya ukaguzi, utunzaji wa kumbukumbu na taarifa za fedha.

Je, Baytulmaal ilikuwepo wakati huo?

Ni muhimu kuepuka mkanganyiko wa kihistoria. Katika kipindi cha Mtume, tayari kulikuwa na ukusanyaji na usimamizi wa mali, pamoja na maafisa waliotekeleza majukumu hayo.

Hata hivyo, mfumo wa Baytulmaal kama hazina pana na taasisi ya kudumu ya kusimamia mapato na matumizi ya umma uliendelea kukua na kuimarika katika vipindi vilivyofuata.

Kwa hiyo, kipindi cha Mtume kiliweka misingi ya kisheria na kiutendaji ya usimamizi wa Zaka, ambayo baadaye iliendelezwa katika mfumo mpana wa hazina ya umma.

Maendeleo ya Baytulmaal wakati wa Maswahaba

Kipindi cha Abu Bakr al-Siddiq (Allah amridhie), 632–634

Baada ya kufariki kwa Mtume, baadhi ya makabila ya Kiarabu yalipinga kulipa Zaka au yakajitenga na mamlaka ya Madina.

Abu Bakr alisimamia msimamo kwamba Zaka ni wajibu wa lazima, na akachukua hatua dhidi ya waliokataa kuitoa katika mazingira yaliyohusika. Kipindi hiki kilithibitisha kuwa Zaka si jambo la hiari linaloweza kuachwa bila sababu ya kisheria. Pia kiliimarisha uhusiano kati ya wajibu wa kidini, mamlaka ya umma na ustawi wa jamii.

Kipindi cha Umar ibn al-Khattab (Allah amridhie), 634–644

Katika zama za Umar, eneo la dola ya Kiislamu lilipanuka kwa kiasi kikubwa. Mapato ya umma yaliongezeka, pamoja na mahitaji ya utawala, ulinzi, ustawi wa jamii na usimamizi wa rasilimali.

Mfumo wa hazina ya umma uliimarika zaidi, ukiambatana na kumbukumbu za mapato, matumizi na malipo kwa makundi mbalimbali.

Mfumo wa Diwan, uliotumika kutunza kumbukumbu za utawala na mgao, uliimarika katika utawala wake.

Huu ni mfano wa namna usimamizi wa mali ulivyotoka katika ukusanyaji na ugawaji na kuelekea kwenye utawala wa kifedha uliopangwa zaidi.

Kipindi cha Uthman ibn Affan (Allah amridhie), 644–656

Katika kipindi hiki, dola ya Kiislamu iliendelea kupanuka na shughuli za kiuchumi zikazidi kuwa pana. Masuala ya ukusanyaji wa mapato, usimamizi wa mali na uhusiano kati ya mali binafsi na wajibu wa Zaka yaliendelea kujadiliwa na kushughulikiwa.

Kwa upande wa Zaka, ni muhimu kutofautisha mali ambazo mtu anaweza kuzisimamia na kuzitolea Zaka mwenyewe na mapato mengine ya umma yanayosimamiwa na mamlaka.

Kipindi cha Ali ibn Abi Talib (Allah amridhie), 656–661

Katika kipindi cha Ali, masuala ya uadilifu, haki na matumizi ya mali ya umma yalikuwa muhimu sana kutokana na changamoto za kisiasa zilizokuwepo.

Urithi muhimu wa kipindi hiki ni msisitizo wa uadilifu katika uongozi na wajibu wa kusimamia mali za umma bila upendeleo. Haya ni maadili yanayopaswa kuwa msingi wa taasisi yoyote ya Zaka.

Baytulmaal baada ya Makhalifa Waongofu

Baada ya zama za Makhalifa Waongofu, dola za Kiislamu ziliendelea kupanuka, huku mapato na majukumu ya serikali yakiongezeka.

Mfumo wa hazina ya umma uliendelea kuhusishwa na mapato mbalimbali, yakiwemo Zaka, Kharaj na mapato mengine yaliyokubalika kisheria katika mazingira ya wakati huo.

Katika vipindi tofauti vya historia ya Kiislamu, kulikuwa na tofauti katika namna mapato yalivyokusanywa, mamlaka zilivyopangwa na mali zilivyogawanywa. Kwa hiyo, si sahihi kudhani kuwa kila dola ya Kiislamu ilikuwa na mfumo mmoja usiobadilika wa Baytulmaal.

Hata hivyo, misingi muhimu ilibaki kuwa usimamizi wa mali za umma kwa uaminifu, kulinda Zaka na kuitumia kwa mujibu wa hukumu zake, kuwafikia wahitaji kwa haki na kuhakikisha wasimamizi wanawajibika kwa matumizi ya rasilimali.



Wahitimu kidato cha 4 Bagamoyo wausiwa maadili na kutafuta elimu

WAHITIMU wa kidato cha nne wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani, wameaswa kuzingatia maadili, kuendeleza elimu na kutumia maarifa waliyopata shuleni kujenga maisha yenye manufaa kwa familia, jamii na taifa.

Nasaha hizo zilitolewa na viongozi wa dini na Serikali katika mahafali yaliyoandaliwa na TAMSYA Mkoa wa Pwani, Kanda A, kwa wahitimu wa shule za sekondari wilayani humo.

Mgeni rasmi, Ibrahim Gama, aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Shaibu Ndemanga, aliwapongeza wahitimu na kuwataka kuishi kwa nidhamu. Pia aliwahimiza wazazi kusimamia malezi na kuwajengea watoto maadili mema.



Kiongozi wa Idara ya Elimu ya TAMSYA, Shabani Thadeo, aliwahimiza wanafunzi kupenda somo la dini, huku akiwasihi wasichana kuzingatia mavazi ya staha yanayokidhi masharti ya hijabu.

Mshauri wa uongozi wa TAMSYA Pwani, Hassan Juma, aliwasilisha salamu za Mkuu wa Mkoa na kuwapongeza wanafunzi kwa nidhamu. Aliwataka wazazi kuwapeleka wahitimu katika kambi za mafunzo ya ujasiriamali zilizoandaliwa na jumuiya hiyo.

Mwalimu wa Sekondari ya Zinga, Kassim Hassan, aliwashauri wahitimu kuwasaidia wazazi katika shughuli za uzalishaji na kuweka akiba ya ada wakati wakisubiri matokeo. Aliwahimiza wavulana kuendelea na masomo.

Mwalimu Malkia Shakiru aliwataka wazazi kulea watoto katika maadili yenye manufaa kwa jamii, na wahitimu kutekeleza waliyofundishwa.

Diwani wa Kata ya Kiromo, Salumu Mikugo, alisema elimu ni msingi wa maisha, akiwataka wahitimu kuitumia kuleta matokeo chanya. Aliwasihi wazazi na walezi kuwasaidia watoto kutimiza ndoto zao.

Kwa upande wake, mhitimu Omary Jabiri aliwashukuru viongozi kwa nasaha na kuwasihi Waislamu kuwa na nia njema katika shughuli zao.



Saudi Arabia yasaidia waathirika 75,000 wa tetemeko Indonesia

Kituo cha Misaada na Huduma za Kibinadamu cha Mfalme Salman (KSrelief) cha Saudi Arabia na Taasisi ya Taifa ya kusimamia Zakat nchini Indonesia (BAZNAS) wamewapatia msaada wa chakula na vifaa vya afya zaidi ya watu 75,000 walioathiriwa na tetemeko kubwa la ardhi huko Flores nchini Indonesia.

Msaada huo umetolewa wakati maelfu ya familia zikiendelea kuishi nje ya makazi yao baada ya tetemeko la ardhi mwezi Agosti lenye ukubwa wa 7.7 na kusababisha vifo vya watu wasiopungua 150 na kujeruhi zaidi ya 1,600, huku nyumba zaidi ya 119,000 zikiharibiwa.

Taasisi hizo zilisambaza vifurushi 15,000 vya chakula na vifaa binafsi vya afya 15,000 vyenye thamani ya takribani dola milioni moja za Marekani sawa na shilingi za Tanzania Bilioni 2.6.

Takwimu za mamlaka zinaonesha zaidi ya watu 28,000 bado hawajarejea katika makazi yao. BAZNAS imesema misaada hiyo ni muhimu katika kuharakisha hatua za kuwarejeshea waathirika maisha ya kawaida, hasa familia ambazo zimepoteza makazi na vyanzo vya kipato.

KSrelief na BAZNAS zimekuwa zikishirikiana tangu mwaka 2022 kutoa misaada ya chakula na mahitaji mengine kwa jamii zenye uhitaji nchini Indonesia.

Nchi za Kiarabu, za Kiislamu na AU waunganisha nguvu kwa Palestina

Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Nchi za Kiarabu na Jumuiya ya Ushirikiano wa Kiislamu (OIC) zimekubaliana kuimarisha uratibu wa kidiplomasia na kisheria ili kuongeza ushawishi wa pamoja katika kutafuta suluhisho la kudumu la mgogoro wa Palestina. Makubaliano hayo yametokana na mkutano wa pamoja uliofanyika katikati ya wiki jijini Addis Ababa, Ethiopia uliojadili namna ya kuoanisha misimamo yao, kutekeleza maazimio ya mikutano ya kimataifa na kuongeza juhudi za kuitambua Palestina kama taifa huru.

Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika, Balozi Moussa Mohamed Omar amesisitiza msimamo wa Afrika wa kuunga mkono taifa huru la Palestina kwa kuzingatia mipaka ya Juni 4, 1967, huku Jerusalem Mashariki ikiwa mji mkuu wake, msimamo unaotokana na misingi ya kujitawala, haki na kuheshimu sheria za kimataifa.

Kwa upande wa OIC, Balozi Assem Hanafi amesisitiza umuhimu wa kuwalinda raia, kuruhusu misaada ya kibinadamu kuingia Gaza bila vikwazo na kuunga mkono shughuli za Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi wa Palestina (UNRWA).

Pia alitoa wito wa kuimarishwa kwa hatua za kisheria dhidi ya ukiukaji wa haki za Wapalestina.

Mkutano huo ulijadili maandalizi ya mpango wa pamoja wa utekelezaji wa mwaka 2027.



Trump, Natanyahu hoi katika uchaguzi, Waislamu wang'ara US

Rais Donald Trump wa Marekani na Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu wa Israel wamepata pigo kubwa la kisiasa baada ya vyama na miungano yao kushindwa katika uchaguzi, huku vita vya Gaza na Iran vikitajwa kuchangia kuongezeka kwa upinzani dhidi yao.

Nchini Marekani, Chama cha Democratic kimeshinda uchaguzi wa katikati ya muhula wa Novemba 3, 2026, na kutwaa udhibiti wa Baraza la Wawakilishi na Seneti kutoka kwa Republican.

Democrats wamejihakikishia angalau viti 54 kati ya 100 vya Seneti dhidi ya 44 vya Republican, huku matokeo ya Alaska na Mississippi yakiendelea kusubiriwa. Pia wamechukua zaidi ya viti 40 vya Republican katika Baraza la Wawakilishi.

Democrats wameshinda viti muhimu vya Seneti katika majimbo ya Texas, Kansas, Ohio, Iowa, North Carolina, South Carolina na Maine.

Matokeo hayo yanapunguza nguvu za Trump katika miaka miwili iliyosalia ya urais wake, huku Democrats wakipata uwezo mkubwa wa kuzuia miswada, kuchunguza serikali na kushinikiza mabadiliko ya sera.

Ushindi huo unahusishwa na kutoridhika kwa wapiga kura kuhusu gharama za maisha, mfumuko wa bei, uhamiaji na athari za vita dhidi ya Iran.

Waislamu waandika historia

Katika uchaguzi huo, Abdul El-Sayed, mwanasiasa mwenye asili ya Misri, ameandika historia kwa kuwa Muislamu wa kwanza kuchaguliwa katika Seneti ya Marekani, baada ya kumshinda Mike Rogers wa Republican jimboni Michigan.

El-Sayed alikuwa miongoni mwa wagombea waliokosoa msaada wa kijeshi wa Marekani kwa Israel.

Kwa mujibu wa Baraza la Mahusiano ya Marekani na Uislamu (CAIR), angalau Waislamu 97 wameshinda nafasi mbalimbali za uongozi, wakiwemo sita waliochaguliwa katika Baraza la Wawakilishi.

Netanyahu apoteza wingi bungeni

Nchini Israel, uchaguzi wa Oktoba 27 umeuacha muungano wa Netanyahu na viti 53 kati ya 120 vya Bunge, pungufu ya viti 61 vinavyohitajika kuunda serikali. Chama chake cha Likud kimepata viti 27, upinzani unaoongozwa na Gadi Eisenkot viti 48 na vyama vinavyoongozwa na Waarabu viti 19.

Rais Isaac Herzog amempa Eisenkot nafasi ya kujaribu kuunda serikali, huku Netanyahu akiendelea kuongoza serikali ya mpito.

Vita vya Gaza, Iran vyawagharimu

Mchambuzi Haydar Oruç, akiandika katika gazeti la Daily Sabah, anasema matokeo hayo yanaonyesha gharama za kisiasa za ushirikiano wa Trump na Netanyahu.

Anasema Trump aliingia madarakani akiahidi kufufua uchumi na kumaliza vita, lakini mapigano dhidi ya Iran na kupanda kwa gharama za nishati kumeongeza upinzani dhidi yake.

٣٠ جُمَادَى الأُولَى ١٤٤٨ هـ

DARASA LA WIKI



SHEIKH
Seif Ruga
0712 690 811

Chimbuko la imani za mikosi katika mwezi wa Safar

Uislamu unapinga imani potofu za mikosi na ishara za bahati mbaya ambazo zimekuwa zikirithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Badala yake, unahimiza kumtegemea Allah na kuwa na yakini kuwa kila jambo hutokea kwa uamuzi na uwezo wake.

Kutokana na imani potofu, baadhi ya watu huingiwa na hofu ya kupata mikosi wanapokutana na watu fulani, wanapozungumza na watu wengine au wanapovaa aina fulani za nguo. Wengine huamini kuwa kusikia sauti za baadhi ya ndege na wanyama, kama vile bundi, kunguru na mbwa ni ishara ya kutokea kwa mikosi.

Aidha, wapo wanaoamini kuwa baadhi ya namba na rangi huashiria mikosi, Wengine hufikia hatua ya kukataa kusafiri katika siku fulani za juma au mwezi kwa madai kuwa siku hizo hazina bahati na zinaweza kuwaletea mikosi.

Vilevile, baadhi ya watu wanaamini kuwa mwezi wa Safar (Mfungo tano), ambao ni mwezi wa pili katika Kalenda ya Kiislamu ni mwezi unaoambatana na mikosi.

Kutokana na imani hiyo, watu hao huepuka kufanya mambo mbalimbali, ikiwamo kufunga ndoa, kutembeleana na kusafiri katika kipindi chote cha mwezi huo. Aidha, baadhi ya watu huepuka kufanya mikutano ya kusuluhisha migogoro kwa madai kuwa mwezi huo hauna bahati.

Imani hiyo ilikuwapo tangu zama za Ujahiliya (kabla ya kuja kwa Nabii Muhammad – rehema na amani za Allah zimshukie). Kwa masikitiko makubwa, baadhi ya Waislamu bado wanaendelea kushikilia imani hiyo hadi leo.

Katika makala hii, tutaangazia dalili za kisharia zinazopinga imani za mikosi na kueleza msimamo wa Uislamu kuhusu suala hili. Kama alivyoumba binadamu, wanyama, mimea na vitu vingine vyote vilivyomo ulimwenguni, ndivyo pia Allah alivyoumba miezi, siku na nyakati.

Allah anasema: “Hakika idadi ya miezi mbele ya Mwenyezi Mungu ni miezi kumi na miwili, katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu tangu siku alipoumba mbingu na ardhi. Kati ya hiyo, iko minne Mitakatifu. Hiyo ndiyo dini iliyonyooka. Basi msijidhulumu nafsi zenu katika miezi hiyo...” [Qur’an, 9:36].

Wanazuoni wa tafsiri ya Qur’an wameeleza kuwa mpangilio huo wa miezi ulithibiti tangu Allah alipoumba dunia na nyakati. Miezi hiyo iliandikwa katika Al–Lawh Mahfudh (Ubao uliohifadhiwa) tangu alipoumba ulimwengu huu, na Allah akawafahamisha Manabii wake mpangilio wake.

Katika kufafanua kauli ya Allah: “Basi msijidhulumu nafsi zenu katika miezi hiyo”, mwanazuoni nguli wa tafsiri ya Qur’an, Ibn Kathir amenukuu maelezo mbalimbali kutoka kwa Sahaba mtukufu, Ibn Abbas (Allah amridhie).

Katika maelezo yake ya kwanza, Ibn Abbas alisema kuwa katazo hilo linahusu miezi yote. Katika maelezo mengine alifafanua kuwa miezi yote inahusika, lakini Allah ameitenga miezi minne na kuipa utukufu wa pekee.

Imani ya kuhusisha ishara fulani na mikosi ilikuwa sehemu ya mila na itikadi za watu wa zama za Ujahiliya. Hata Manabii na Mitume wa Allah (amani iwe juu yao) hawakusalimika na imani hizo potofu. Baadhi ya watu wao waliwahusisha na mikosi iliyowapata, wakiamini kuwa wao ndio chanzo cha nuksi hizo.

Kwa mfano, watu wa Thamud, ambao Allah alimtuma kwao Nabii Swaleh (amani iwe juu yake) walimwambia: “Tumepata nuksi kwa sababu yako na kwa wale walio pamoja nawe.” [Qur’an, 27:47].

Uislamu umekuja na itikadi iliyo wazi inayolenga kung’oa mizizi ya imani potofu na dhana za kishirikina ambazo zimetawala maisha ya watu kwa muda mrefu.

Mtume (rehema na amani ya Allah zimshukie) amesema: “Hakuna maambukizi ya maradhi yanayotokea yenyewe (bila ya idhini ya Allah), hakuna kuamini mikosi, hakuna mkosi wa mwezi wa Safar (Mfungo tano), wala kuamini kuwa (kumuona) bundi ni ishara ya mkosi.”

Katika hadith nyingine Mtume amesema: “Kuamini mikosi ni shirk.” [Abu Daudi, Tirmidhi na Ibn Majah]. Vilevile, imepokewa kutoka kwa Ikrima kwamba alipokuwa kwa Ibn Abbas (Allah awaridhie wote), ndege mmoja alipita huku akilia. Mtu mmoja aliyekuwa pamoja nao akasema: “Kheri, kheri!” Ibn Abbas akamwambia: “Ndege huyu hana kheri wala shari.”

Hapo zamani, watu waliingiwa na hofu kubwa walipomwona bundi akitua juu ya nyumba zao, wakiamini kuwa tukio hilo lilikuwa ishara ya kifo chao au cha mmoja wa wanafamilia wao.

Muislamu hapaswi kutawaliwa na hofu na mashaka yanayotokana na imani hizo potofu. Badala yake, anapaswa kuzipinga na kuendelea na shughuli zake halali bila kuruhusu dhana za kishirikina kuathiri imani yake.

Mtume (rehema na amani ya Allah zimshukie) ameelekeza kuwa mwenye kuamini mkosi aendelee na jambo lake, mwenye husuda amuombe Allah msamaha, na mwenye dhana mbaya asiifuatilie kwa kuichunguza ili kuithibitisha.

Muislamu hapaswi kuruhusu hisia zitawale maisha yake, bali amtegemee Allah na ajiepushe na imani zisizo na msingi.

وقف

NA
Idara ya elimu Awqaf

MAKALA ZA WAQF

Waqf, huku ndipo pa kuwekeza!

Maeneo 4 ya kipaumbele Waqf unaweza kuleta mabadiliko Tanzania

SEHEMU YA
9

Waqf ni miongoni mwa mifumo muhimu ya Kiislamu yanayoweza kutumika kujenga maendeleo endelevu ya jamii. Hata hivyo, uwezo wake bado haujatumika kikamilifu katika kukabiliana na changamoto za elimu, afya, uchumi na huduma za kijamii. Makala hii inaangazia maeneo manne ya kipaumbele ambayo Waislamu Tanzania Bara wanaweza kuelekeza mali zao za Waqf ili kujenga taasisi imara na kuleta mabadiliko yanayodumu kwa vizazi vijavyo.

Mosi: Elimu, msingi wa mabadiliko ya kudumu

Elimu ni nyenzo muhimu katika kujenga uwezo wa mtu binafsi na jamii kwa ujumla. Hata hivyo, historia ya elimu kwa Waislamu Tanzania ina changamoto zake, zikiwemo upungufu wa taasisi zenye rasilimali za kutosha na mifumo endelevu ya kuziendesha.

Waqf unaweza kusaidia kubadili hali hii kwa namna kadhaa ikiwemo kuanzisha na kuimarisha shule bora za Kiislamu zenye viwango vya juu vya kitaaluma, pamoja na kutoa nafasi kwa wanafunzi kutoka familia zenye kipato cha chini.

Namna nyingine ni kufadhili elimu ya juu hasa wa fani muhimu kama udaktari, uhandisi, sheria, sayansi ya data na teknolojia ya habari na mawasiliano. Hii inaweza kufanyika kupitia waqf wa fedha (cash waqf).

Eneo jingine katika elimu ni kuboresha maslahi ya walimu, maimamu, waadhini na wahudumu wengine wa misikiti na madrasa kwa kuweka mifumo ya malipo na posho za uhakika kwao ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa utulivu na ufanisi.

Muhimu pia kuwekeza katika elimu ya ufundi kwa kuanzisha vituo vya mafunzo ya ufundi na stadi za kazi (TVET) ili kuwajengea vijana uwezo wa kujiajiri na kushiriki katika soko la ajira.

Pili: Mifumo endelevu ya huduma za Afya

Huduma za afya ni hitaji la msingi ambalo linapaswa kupatikana kwa kila mwanajamii. Katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara, wananchi bado wanakabiliwa na changamoto za umbali wa vituo vya afya, upungufu wa vifaa na gharama za matibabu.

Waqf unaweza kuchangia suluhisho kwa namna kadhaa ikiwemo kuanzisha zahanati na vituo vya afya vinavyoendeshwa kwa misingi ya waqf, vikitoa huduma kwa gharama nafuu na kusaidia wagonjwa wasio na uwezo.

Namna nyingine ni kuweka mfuko wa dawa na matibabu kwa kuanzisha mfuko maalumu wa kusaidia wagonjwa wanaohitaji matibabu ya muda mrefu, yakiwemo ya saratani na magonjwa ya figo.

Eneo jingine la kipaumbele katika afya ni kuimarisha afya ya mama na mtoto kwa kuwekeza katika huduma za uzazi, wodi za wajawazito na huduma za watoto ili kupunguza vifo vinavyoweza kuzuilika.

Uzoefu wa taasisi kama Aga Khan Health Services unaonesha umuhimu wa kujenga mifumo ya afya yenye taasisi, rasilimali na usimamizi endelevu inayoweza kuhudumia jamii kwa muda mrefu.

Tatu: Uwezeshaji wa kiuchumi na kifedha

Changamoto ya ukosefu wa mitaji ni kikwazo kikubwa kwa wafanyabiashara wadogo, vijana na makundi yenye kipato cha chini. Waqf unaweza kuwa chombo cha kuwainua kiuchumi badala ya kuwafanya waendelee kutegemea misaada.

Maeneo ya uwekezaji ni pamoja na waqf wa fedha (cash waqf) kwa ajili ya kuwekeza fedha katika miradi au bidhaa za uwekezaji zinazokubalika kwa mujibu wa Sharia, kisha kutumia mapato yake kutoa mikopo isiyo na riba (Qardh Hasan) kwa wajasiriamali.

Tuangalie pia matumizi ya Waqf katika zana za uzalishaji kwa kununua matrekta, mashine za usindikaji, vifaa vya ujenzi na vyombo vya usafirishaji ambavyo vitatumika kuzalisha kipato na kutoa fursa za ajira.

Majengo ya biashara ni eneo jingine la kupewa kipaumbele kw ajili ya uwezeshaji wa kiuchumi ambapo kujengwe maduka, masoko na majengo ya kupangisha katika maeneo yenye shughuli nyingi za kiuchumi. Mapato yake yaelekezwe katika huduma za jamii na kuendeleza mali ya waqf.

Ukuaji wa huduma za kifedha zinazozingatia misingi ya Kiislamu nchini, kupitia taasisi mbalimbali za fedha, unaweza kutoa fursa za ushirikiano katika uwekezaji huu, kwa kuzingatia masharti ya Sharia na usalama wa mtaji.

Nne: Hifadhi ya maji na usafi wa mazingira

Maji safi ni hitaji linalogusa afya, elimu na ibada. Katika baadhi ya vijiji, wanawake na watoto hutumia muda mwingi kutafuta maji, hali inayoweza kuathiri masomo, shughuli za uzalishaji na usalama wao.

Waqf unaweza kusaidia katika eneo hili kwa kuchimba, kujenga na kudumisha visima vya maji katika maeneo yenye upungufu mkubwa wa huduma hiyo na vilevile kupanua miundombinu ya maji kwa kusaidia usambazaji wake vijijini na maeneo ya pembezoni.

Sambamba na hayo, ni muhimu pia kuboresha usafi wa mazingira kwa ujenzi wa vyoo bora na kuweka mifumo ya maji safi katika misikiti, madrasa na maeneo ya umma ili kuimarisha afya na usafi unaohitajika kwa ibada.

Hitimisho

Maeneo haya manne yanaonesha kuwa waqf unaweza kuwa zaidi ya mali inayotolewa kwa ajili ya matumizi ya kidini. Unaweza kuwa msingi wa kujenga shule, hospitali, mifumo ya kifedha na miundombinu inayohudumia jamii kwa muda mrefu.

وقف

UCHAMBUZI/ MAONI

NA
Mwandishi Wetu

Tume ya Waqf Tanzania Bara: Suluhisho au tatizo jingine?

Katika miezi ya hivi karibuni, hatma ya rasilimali na mali za kiroho na kijamii imerejea kwa kishindo kwenye meza ya mazungumzo ya umma nchini Tanzania.

Kuanzia kwenye ukumbi wa Bunge kupitia angalizo la Mbunge Sabreena Hamza Sungura, hadi kwenye mijadala ya wazi iliyoibuliwa na aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, na wachambuzi huru kama Khalfan Abdallah Salim, suala la kutokuwepo kwa Tume ya Waqf Tanzania Bara limeonekana kuwa donda ndugu linalohitaji utatuzi wa haraka.

Mjadala huu unagusa kiini cha uchumi wa jamii, uwajibikaji na mgawanyiko uliopo kati ya matakwa ya kisheria ya nchi na uhalisia wa utawala wa rasilimali za kidini.

Katika mijadala ya Bunge, wabunge wamekuwa wakinyoosha kidole kwenye pengo kubwa linalosababishwa na kutokuwepo kwa chombo rasmi cha kusimamia Waqf chini ya Sheria ya Mirathi na Usimamizi wa Mali (Cap. 352) ya mwaka 1963.

Sheria inatambua uwepo wa Waqf na kutoa fursa ya kuwepo kwa Tume, kama ilivyokuwa katika sheria za ukoloni za mwaka 1953. Hata hivyo, kutokuwepo kwake kumewafanya walezi binafsi kujiamulia mambo, hali inayosababisha mali nyingi za misikiti, mashamba na majengo ya hisani kudhulumiwa au kugeuzwa mali binafsi.

Pigo kubwa la kihistoria lilitokea wakati wa mchakato wa kuchukuliwa na kuhamishwa kwa mali za Waqf zilizokuwa chini ya Jumuiya ya Waislamu ya Afrika Mashariki (EAMWS).

Kutokana na kutotumika kwa nyaraka, takwimu sahihi, hati miliki na vitabu vya kumbukumbu wakati huo, mali nyingi hazikukabidhiwa kwa utaratibu unaoeleweka, na ziliishia kupotea mikononi mwa wajanja. Viwanja, mashamba, shule na majengo yaligeuzwa kimyakimya kuwa mali binafsi kwa kukosa chombo wala kumbukumbu za kusimamia urithi huo wa jamii.

Hapa ndipo hoja ya Prof. Mussa Assad na wachambuzi wa masuala ya kiuchumi inapopata uzito. Tofauti na Zanzibar, ambayo ina Tume ya Waqf inayofanya kazi kikamilifu chini ya Sheria Namba 2 ya mwaka 2007, Tanzania Bara imebaki katika mfumo uliotawanyika bila miongozo thabiti.

Hali hii inasababisha hasara kubwa ya kiuchumi, ambapo mali zilizopo hazizalishi faida inayolingana na thamani yake halisi kutokana na ukosefu wa viwango vya ukaguzi wa kitaalamu na mifumo ya uwazi.

Hata hivyo, jitihada za kuunda Tume ya kiserikali zimekuwa zikigonga ukuta wa kikatiba. Chini ya Ibara ya 19 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchi yetu haina dini rasmi (secular state). Msimamo wa kiserikali na kibunge umekuwa ukisisitiza kuwa mambo ya dini yashughulikiwe na dini yenyewe.

Mjadala huu unashabihiana pia na mjadala wa Mahakama ya Kadhi au tukio la kihistoria la Zanzibar kutaka kujiunga na Jumuiya ya Ushirikiano wa Kiislamu (OIC) mapema miaka ya 1990. Wakati Zanzibar iliona fursa hiyo kama njia ya kupata mtaji na misaada ya kiuchumi kupitia Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IDB), Serikali Kuu ilipinga hatua hiyo kwa sababu za kikatiba na kiusalama.

Kutotolewa kwa Kanuni za Utekelezaji (Regulations) na mawaziri husika kwa miaka nenda miaka rudi hakujatokea kwa bahati mbaya, bali kunatokana na mambo makuu manne.

Kwanza, ni hofu ya kugongana na Katiba kuhusu nchi isiyo na dini rasmi. Pili, uwepo wa msimamo imara wa upande wa pili kwamba “dini iendeshwe na dini yenyewe” ili kuepuka misuguano ya kijamii. Tatu, kuwepo kwa njia mbadala za kisheria kupitia Kabidhi Wasii Mkuu (RITA), chini ya Sheria ya Usajili wa Wadhamini (Trustees’ Incorporation Act), inayoruhusu misikiti na taasisi kusajili bodi zao za udhamini. Nne, kukosekana kwa msukumo thabiti wa kisiasa (political will).

Hata pale nchi ilipoongozwa na marais Waislamu, hawakuchukua hatua za kuanzisha Tume hiyo kutokana na mtego mzito wa kisiasa.

Rais anapoapishwa, huapa kulinda Katiba, na kuunda chombo cha kiserikali cha huduma za kidini kungetafsiriwa kwa makusudi kama upendeleo, jambo linaloweza kuzua misuguano. Ili kulinda umoja wa kitaifa na kuepuka tuhuma za udini, viongozi hao waliepuka kuingiza dola kwenye migogoro ya kiimani.

Je, Tume ya Waqf sasa bado ina ulazima?

Kwa kuwa msimamo wa kisheria na kisiasa hautoi mwanya wa serikali kuunda Tume ya Waqf Bara, mtazamo mpya unaibuka: Hakuna haja ya Tume ya kiserikali. Badala yake, hakuna haja ya kuendelea kuitegemea au kuisubiri.

Kwa takribani karne moja, tangu 1923, Tume ya kiserikali haikuwepo. Sasa ije kuleta nini zaidi ya urasimu na hofu ya wanasiasa na vyombo vya serikali kuingilia zaidi rasilimali za Waqf za Waislamu?

Mali ziliathirika wakati wa Operesheni Vijiji na wakati wa Uchukuaji wa Majengo wa mwaka 1971 (Building Acquisition Act, 1971). Kwa msingi huo, hoja ya kupinga kabisa ulazima wa kuwepo kwa Tume ya Waqf inayoendeshwa au kusimamiwa na serikali ina mashiko zaidi.

Wahusika na wachambuzi wa hoja na msimamo huu wanakumbusha kuwa serikali haipaswi kutumia mamlaka au kodi za wananchi wote kuunda vyombo vya kiimani, kwani kufanya hivyo kunaweza kuzua mkwamo mkubwa wa kisheria na hofu ya wanasiasa kuingilia rasilimali za Kiislamu.

Hii ni kwa sababu, kwanza, ya uwepo wa misingi ya nchi isiyo na dini rasmi na matakwa ya kikatiba. Pili, madhila ya taasisi za kiserikali wanapotaka kusajili taasisi, ambapo visingizio hutolewa, ikiwemo vya uchunguzi.

Uzoefu wa karne moja bila ya kuwa na Tume unatukumbusha kuwa mali za Waqf ni amana nzito, na kwa mfumo wa sasa si lazima kuwe na Tume ya Serikali ili kuleta tija katika mambo ya dini ambayo yana wenyewe.

Wenyewe wajipange kwa taqwa, uaminifu na weledi wa kitaalamu kutoka ndani ya jamii yenyewe kuzilinda mali zilizowekwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na jamii, na kuzuia historia ya kupotezwa kwa mali za Waqf isijirudie.

Dhana hii ya kujisimamia ina nguvu zaidi wakati huu na inapaswa kutetewa mwanzo hadi mwisho. Ipiganiwe hoja kwamba Waqf ni ibada yetu, na tuachiwe uhuru wa kuabudu uliopo kikatiba.

٣٠ جُمَادَى الأُولَى ١٤٤٨ هـ

فتاوى



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Kinyesi cha binadamu, nguruwe kama mbolea ya kurutubisha mazao

Swali: Kuna baadhi ya wakulima wanaotumia kinyesi cha binadamu na nguruwe kama mbolea ya kurutubisha mashamba yao ili kuongeza uzalishaji wa mazao. Wengine hutumia kinyesi hicho kikiwa kimechanganywa na udongo, huku wengine wakikitengeneza kuwa mbolea kupitia mifumo mbalimbali ya uchakataji. Je, kwa mujibu wa Sharia ya Kiislamu, inaruhusiwa? Na je, inaruhusiwa kula mazao yanayozalishwa kwa kutumia mbolea hizo?

Jawabu: Kwa hakika, Uislamu ni dini inayozingatia usafi, usalama na manufaa ya mwanadamu. Sharia imeweka kanuni zinazohifadhi maisha, afya, mali na mazingira.

Kwa msingi huo, matumizi ya vitu mbalimbali katika shughuli za kilimo yanapaswa kuchunguzwa kwa kuzingatia hukumu zake za Kisharia pamoja na madhara au manufaa yanayotokana na matumizi hayo.

Ili kulijibu swali hili kwa usahihi, tunahitaji kuangalia mambo matatu: hukumu ya kinyesi cha binadamu na nguruwe, hukumu ya kukitumia kama mbolea, na hukumu ya mazao yanayozalishwa kwa kutumia mbolea hizo.

Kwanza: Hukumu ya kinyesi cha binadamu na nguruwe

Kwa mujibu wa wanazuoni wengi, kinyesi cha binadamu ni najisi. Kadhalika, nguruwe ni miongoni mwa wanyama ambao Sharia imeharamisha ulaji wao, na wanazuoni wengi wanahesabu kinyesi chake kuwa najisi.

Hata hivyo, kuwepo kwa najisi katika kitu hakumaanishi kwamba matumizi yake yote yanakuwa yameharamishwa. Wanazuoni wamejadili tofauti kati ya matumizi ya kitu najisi kwa namna inayohusisha kula au kunywa, na kukitumia kwa manufaa mengine yasiyohusisha kula au kunywa.

Pili: Hukumu ya kutumia kinyesi kama mbolea ya kilimo

Wanazuoni wamekhitalifiana kuhusu kutumia vitu najisi katika kurutubisha ardhi.

Kauli ya kwanza: Inajuzu kutumia mbolea najisi.

Hii ndiyo kauli ya jumhuri ya wanazuoni kutoka katika madhehebu ya Hanafi, Maliki na Shafi'i, pamoja na baadhi ya wanazuoni wa Hanbali.

Imam Ibn al-Qayyim (Allah amrehemu) amenukuu kauli hii katika kitabu chake Zad al-Ma'ad, akisema: "Jumhuri ya wanazuoni wamejuzisha kunufaika na samadi najisi katika kurutubisha ardhi kwa ajili ya kilimo, matunda na mboga, pamoja na kwamba samadi hiyo ni najisi yenyewe." [Rejea: Zad al-Ma'ad, 5/664]

Vilevile, Imam Nawawiy (Allah amrehemu) katika Al-Majmuū' Sharh al-Muhadhdhab, 4/448, amesema: "Inajuzu kurutubisha ardhi kwa kutumia samadi najisi."

Hii inaonesha kwamba wanazuoni hao wametofautisha kati ya hukumu ya kinyesi chenyewe na hukumu ya kukitumia kama mbolea kwa ajili ya manufaa ya ardhi.

Kauli ya pili: Msimamo mashuhuri wa madhehebu ya Hanbali.

Wanazuoni wa Hanbali wana msimamo tofauti kuhusu hukumu ya mazao yanayorutubishwa au kumwagiliwa kwa vitu najisi.

Imam al-Bahuti katika kitabu chake Kasshaf al-Qina', juzuu ya 6, ukurasa wa 194, amesema: "Mazao na matunda yaliyomwagiliwa kwa kitu najisi au kurutubishwa kwa mbolea najisi yanakuwa najisi na yanakuwa haramu kuliwa kwa sababu hiyo."

Hata hivyo, ameeleza kuwa mazao hayo yanaweza kutakasika ikiwa baadaye yatamwagiliwa kwa maji safi yanayoondoa athari ya najisi.

Ni muhimu kufahamu kuwa msimamo huu hauhusu kumwagilia mimea kwa maji najisi pekee, bali pia unahusu kurutubisha ardhi kwa kutumia mbolea najisi.

Tatu: Hukumu ya mazao yanayozalishwa kwa kutumia

فتاوى

Kinyesi cha binadamu, nguruwe kama mbolea ya kurutubisha mazao

mbolea hizo

Hili ndilo eneo lenye umuhimu mkubwa katika swali letu.

Kwa mujibu wa jumhuri ya wanazuoni, mazao yaliyokuzwa katika ardhi iliyotumia mbolea najisi hayawi najisi kwa sababu hiyo pekee. Hii ni kwa sababu vitu vilivyokuwa najisi vinapochanganyika na udongo na kufyonzwa na mmea, sehemu yake hubadilika na kuwa virutubisho vinavyosaidia ukuaji wa mmea.

Katika kulielezea jambo hili, Ibn Hazm (Allah amrehemu) amesema: "Samadi, kinyesi, mkojo, maji na udongo, vyote hivyo hubadilika ndani ya mtende na kuwa majani na tende." [Rejea: Ibn Hazm, Al-Muhallā, 1/294].

Hoja hii inahusiana na kanuni ya Kisharia inayojulikana kama Al-Istihalah, yaani kubadilika kwa kitu kutoka hali yake ya awali na kuwa kitu kingine chenye sifa na uhalisia tofauti. Kwa hiyo, mazao yaliyopata virutubisho kutokana na mbolea hizo hayahukumiwi kuwa najisi kwa sababu tu chanzo cha baadhi ya virutubisho hivyo kilikuwa najisi.

Hata hivyo, ikiwa kinyesi au uchafu huo utagusa moja kwa moja sehemu ya mmea au tunda, sehemu iliyoathirika inapaswa kuoshwa kabla ya kuliwa.

Nne: Je, matumizi ya mbolea hizo yanaweza kuwa na madhara?

Pamoja na kuruhusiwa kwa matumizi ya mbolea najisi kwa mujibu wa kauli ya jumhuri, ni lazima kuzingatia usalama wa afya ya binadamu.

Inawezekana kinyesi cha binadamu au nguruwe kikawa na vijidudu, vimelea au uchafu wa kemikali unaoweza kusababisha madhara kwa watumiaji wa mazao. Kwa hiyo, kinyesi kinachotumika kama mbolea kinapaswa kufanyiwa uchakataji unaofaa ili kupunguza au kuondoa hatari hizo.

Shirika la Afya Duniani (WHO), katika mwongozo wake wa "Guidelines for the Safe Use of Wastewater, Excreta and Greywater," limeeleza umuhimu wa kutathmini na kudhibiti hatari za vijidudu vinavyoweza kuambukiza kupitia matumizi ya kinyesi na maji taka katika kilimo.

Hili linahusiana na kanuni ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani): "Hakuna kujidhuru wala kumdhuru mwingine."

Kwa hiyo, ikiwa itathibitika kitaalamu kwamba mbolea fulani ina madhara kwa afya ya binadamu, matumizi yake yatakuwa hayaruhusiwi kwa sababu ya madhara hayo, hata kama matumizi ya mbolea najisi kwa asili yake yanajuzu. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.



HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU NA

Na Ukhti Fatima SS
0789 201 383



Profesa: Huduma Fedha za Kiislamu zipunguze pengo matajiri na maskini

NIGERIA — Mtaalamu wa sheria za Kiislamu, Prof. AbdulRazaq AbdulMajeed Alaro, amezitaka taasisi za fedha za Kiislamu kupunguza pengo kati ya matajiri na maskini, kutengeneza ajira na kuhakikisha huduma zake zinaleta haki na ustawi wa jamii, badala ya kujikita katika faida pekee.

Akizungumza katika Mkutano wa Kwanza wa Vijana kuhusu Fedha za Kiislamu, uliofandaliwa na NEXTIF mjini Ilorin, Novemba 5, 2026, Prof. Alaro alisema kufuata masharti ya Sharia pekee hakutoshi bila kuzingatia manufaa ya huduma hizo kwa jamii.

Alisisitiza umuhimu wa kuzingatia malengo makuu ya Sharia (Maqasid al-Sharia), yanayohusisha kulinda dini, maisha, akili, familia na mali.

Alisema taasisi zinapaswa kuchunguza si uhalali wa mikataba pekee, bali pia aina ya biashara zinazofadhiliwa na athari zake kwa jamii.

Prof. Alaro alionya kuhusu kuongezeka kwa tofauti za kiuchumi, akitaja takwimu zinazoonyesha kuwa chini ya asilimia 10 ya watu duniani wanamiliki zaidi ya asilimia 80 ya utajiri.

Alisema fedha za Kiislamu zinapaswa kushughulikia tofauti hizo kwa kufadhili kilimo, elimu, afya, makazi nafuu na biashara ndogo na za kati, hususan kwa wanawake, vijana na wakulima. Pia alihimiza matumizi ya Zaka, Waqf, Sadaka na mikopo isiyo na riba kusaidia wahitaji.

Alikosoa utegemezi mkubwa wa mikataba ya Murabaha, akitaka taasisi ziongeze mifumo ya ushirikiano wa biashara na kugawana faida na hasara, ikiwemo Mudarabah na Musharakah.

Aidha, alisisitiza ushirikiano kati ya wanazuoni wa Sharia na watendaji wa fedha ili kuunganisha uelewa wa hukumu za Kiislamu na uhalisia wa biashara.

Aliwataka vijana kutumia teknolojia kubuni huduma za kifedha zenye maadili na zinazotatua matatizo halisi ya kiuchumi.

Prof. Alaro alisisitiza kuwa ujumuishi wa kifedha haupaswi kuwa lengo la mwisho, bali njia ya kuboresha maisha na kuhakikisha wananchi wengi zaidi wananufaika na maendeleo ya uchumi.

Malaysia yapendekeza kufufua taasisi ya Zaka duniani

ISTANBUL — Malaysia imependekeza kufufuliwa kwa Shirika la Kimataifa la Zaka (IZO) ili kuratibu ukusanyaji na ugawaji wa Zaka duniani, hususan kusaidia nchi maskini za Kiislamu na jamii za Waislamu walio wachache.

Naibu Waziri Mkuu wa Malaysia, Dkt. Ahmad Zahid Hamidi, alisema shirika hilo, lililoanzishwa mwaka 2008, linaweza kupata fedha kutoka nchi tajiri za Kiislamu.

Alisema pia kuna pendekezo la kuchunguza uwezekano wa kutumia riba ambayo wenye amana za fedha zinazotokana na biashara ya mafuta katika benki za kimataifa hawachukui kwa sababu za kidini.

Akizungumza Istanbul, Zahid alisema fedha hizo zinaweza kusaidia makundi manane yanayostahiki Zaka na kuboresha maisha ya Waislamu.

Alisema wazo la kuanzisha shirika hilo lilitolewa awali na marehemu Sheikh Saleh Abdullah Kamel wa Saudi Arabia.

Pendekezo la kulifufua lilijadiliwa pia na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Nchi Nane Zinazoendelea (D-8), Sohail Mahmood, Novemba 6.

Zahid alisema anatarajia suala hilo kujadiliwa katika mikutano ya Jumuiya ya Ushirikiano wa Kiislamu (OIC) na D-8.

Chanzo: Bernama / The Sun Malaysia

Misri, Nigeria na Tunisia zatawala orodha ya benki bora za Kiislamu Afrika

Benki za Kiislamu kutoka Misri, Nigeria na Tunisia zimeongoza kwa idadi katika orodha ya benki 10 za Afrika zilizojumuishwa kwenye viwango vya benki 100 imara zaidi za Kiislamu duniani kwa mwaka 2026.

Kwa mujibu wa tathmini ya TAB Global, Misri na Tunisia zina benki tatu kila moja, Nigeria mbili, huku Kenya na Afrika Kusini zikiwa na benki moja kila nchi.

Abu Dhabi Islamic Bank Egypt imeongoza Afrika kwa kushika nafasi ya 27 duniani, ikifuatiwa na Al Baraka Bank Egypt katika nafasi ya 35.

TAJBank na Jaiz Bank za Nigeria zimeshika nafasi za 62 na 65, huku Gulf African Bank ya Kenya ikishika nafasi ya 73.

Tathmini hiyo imezingatia uimara wa kifedha, faida, ukwasi na ubora wa mali za benki.

Chanzo: Ecofin Agency

Huduma Fedha za Kiislamu zahimizwa kuvuka mipaka ya kitaifa

MALAYSIA — Wataalamu wa fedha za Kiislamu wamezitaka taasisi za sekta hiyo kupanua huduma katika masoko ya kimataifa badala ya kujikita katika nchi zao pekee.

Wito huo ulitolewa katika Jukwaa la Kimataifa la Taasisi za Fedha za Kiislamu, lililoandaliwa na benki ya Standard Chartered mjini Kuala Lumpur.

Washiriki walisema sekta hiyo inahitaji kuunganisha masoko, kuongeza upatikanaji wa mitaji na kuimarisha huduma zinazochochea maendeleo ya uchumi.

NA UKHTI FATIMA



Uelewa wa mteja ndio mafanikio ya biashara yako

Unaweza kuwa na bidhaa bora, teknolojia ya kisasa, wafanyakazi wenye ujuzi na mtaji mkubwa, lakini biashara yako ikashindwa. Sababu inaweza kuwa moja tu: Kutomwelewa mteja.

Hili ni kosa linalofanywa na wajasiriamali wengi. Wanatumia muda na fedha kubuni bidhaa, kupanga bei na kutangaza biashara zao, lakini hawajiulizi kama bidhaa hizo zinatatua matatizo halisi ya wateja.

Mtaalamu wa usimamizi wa bidhaa, Thiago Brant, anasimulia uzoefu alioupata aliposhiriki kutengeneza mfumo wa kidijitali wa kuomba mikopo katika taasisi moja ya fedha.

Timu yake ilikuwa imefanya maandalizi makubwa. Teknolojia ilikuwa tayari na mfumo ulitarajiwa kuzinduliwa.

Walipomwalika mwanamke mmoja kuujaribu, waligundua tatizo ambalo hawakulitarajia kiasi kwamba alihitaji kumwita mwanawe amsaidie.

Hapo timu ilitambua kwamba walikuwa wametengeneza mfumo mzuri kiteknolojia, lakini hawakuzingatia uwezo wa mtumiaji.

Kisa hiki kinafundisha umuhimu wa falsafa inayojulikana kama Customer-Centricity, yaani kuendesha biashara kwa kumweka mteja katika kitovu cha maamuzi. Badala ya kujiuliza tunataka kuuza nini, mfanyabiashara anapaswa kujiuliza mteja anahitaji nini. Ili kutimiza hilo, hizi ni dondoo muhimu za kuzingatia.

Mosi, mfahamu mteja wako

Wateja hutofautiana kwa kipato, umri, elimu, mazingira na matarajio. Bidhaa inayomfaa mtu mmoja huenda isimfae mwingine.

Mfanyabiashara anapaswa kuchunguza mahitaji ya wateja wake badala ya kutegemea mawazo yake mwenyewe.

Kwa mfano, mfumo wa malipo unaofaa vijana waliozoea simu janja unaweza kuwa changamoto kwa wazee wasiofahamu teknolojia.

Pili, sikiliza malalamiko ya wateja

Wafanyabiashara wengine huona malalamiko kama usumbufu. Lakini malalamiko yanaweza kuwa chanzo muhimu cha taarifa kuhusu udhaifu wa biashara.

Mteja anapolalamikia kuchelewa kwa huduma, ubora wa bidhaa au namna anavyohudumiwa, anatoa nafasi ya kufanya maboresho. Muhimu si kusikiliza pekee, bali kuchukua hatua.

Tatu, uza suluhisho, si bidhaa pekee

Wateja wengi hawanunui bidhaa kwa sababu tu zipo sokoni. Wanataka kutatua matatizo au kukidhi mahitaji fulani.

Anayenunua godoro anahitaji usingizi wenye starehe. Anayeingia mgahawani anatarajia chakula kizuri na huduma inayoridhisha. Mfanyabiashara anayeelewa mahitaji hayo ana nafasi nzuri ya kuwavutia na kuwabakiza wateja.

Nne, washirikishe wateja katika kubuni bidhaa

Usisubiri bidhaa iwe tayari ndipo uombe maoni. Waulize wateja wanachohitaji, waruhusu kujaribu bidhaa na chunguza matatizo wanayokutana nayo.

Njia hii inaweza kuzuia matumizi makubwa ya fedha kutengeneza bidhaa ambazo watu hawazihitaji au hawawezi kuzitumia.

Tano, jenga mahusiano ya muda mrefu

Mteja si mtu wa kukupatia fedha leo na kuondoka. Anaweza kuwa mshirika wa biashara yako kwa miaka mingi. Huduma nzuri, uaminifu na kushughulikia malalamiko kwa wakati vinaweza kumfanya arudi tena na kuwashauri wengine kununua kwako.

Hata hivyo, kumweka mteja kwanza hakumaanishi kukubali kila anachotaka. Biashara lazima izingatie ubora, gharama na uwezo wake wa kujiendesha.

Sita, wajenge wafanyakazi wanaojali wateja

Huduma bora haiwezi kutegemea mmiliki wa biashara pekee. Kila mfanyakazi ana mchango katika uzoefu wa mteja. Wafanyakazi wanahitaji mafunzo, motisha na mamlaka ya kushughulikia changamoto bila urasimu usio wa lazima.

Mfanyakazi anayeheshimiwa na kusikilizwa anaweza kuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kuwahudumia wengine.

Saba, endelea kuboresha huduma

Mahitaji ya wateja hubadilika. Teknolojia, ushindani na hali ya uchumi pia hubadilika. Biashara inayofanikiwa leo inaweza kupoteza wateja kesho ikiwa haitafuatilia mabadiliko hayo.

Kwa hiyo, ukusanyaji wa maoni, tathmini ya huduma na ubunifu vinapaswa kuwa shughuli za kudumu.

Nihitimishe kwa kusema mfanyabiashara anayewasikiliza wateja, kuelewa matatizo yao na kuboresha huduma anaweka msingi wa biashara endelevu.

Funzo kuu ni hili: Usitengeneze bidhaa kwanza kisha utafute watu wa kuinunua. Tambua mahitaji ya watu, kisha tengeneza bidhaa inayowafaa.

UCHAMBUZI /MAONI

NA
Abeid Othman
0754 990 083

Wahitimu hawa wametuvua nguo wazazi wa Kiislamu

Wahitimu wa shule wanapofichua pengo la maadili, lawama haziwezi kuwa za vijana pekee; wazazi wa Kiislamu wanapaswa kujiuliza walitimiza kwa kiasi gani dhamana ya malezi waliyopewa na Mwenyezi Mungu.

Malezi ya watoto si jukumu la shule wala madrasa pekee; ni dhamana kubwa inayoanzia nyumbani na ambayo kila mzazi ataulizwa mbele ya Mwenyezi Mungu.

Tukio la hivi karibuni lililohusisha baadhi ya wahitimu wa kidato cha nne waliotoa kauli za matusi na zisizo na staha mitandaoni, limeacha maswali mengi kuhusu malezi ya watoto wetu, hasa katika familia za Kiislamu.

Kilichoongeza uzito wa mjadala huo ni kwamba wengi walioonekana katika tukio hilo, walikuwa wamevaa ushungi, vazi ambalo katika jamii zetu mara nyingi linahusishwa na utambulisho wa mwanamke wa Kiislamu.

Kwa mtu anayethamini maadili ya dini, tukio hilo haliwezi kuchukuliwa kama burudani ya kawaida ya vijana wanaosherehekea kumaliza elimu ya sekondari. Ni jambo linalopaswa kutufanya wazazi, walezi na jamii kwa ujumla tutafakari upya tunavyowalea watoto wetu.

Ni kweli, hatuwezi kutoa hitimisho kwamba kila aliyevaa ushungi katika tukio hilo alikuwa Muislamu. Wala hatuna ushahidi wa kutosha kusema kama yaliyotokea yalikuwa matokeo ya tabia za wahusika wenyewe au kulikuwa na mchezo wa propaganda uliofanywa kwa makusudi ili kuuchafua Uislamu.

Hatutakiwi pia kuingia katika hukumu za jumla dhidi ya mabinti wote waliokuwa katika tukio hilo.

Hata hivyo, kuna jambo ambalo hatuwezi kulikwepa: bado tuna changamoto kubwa ya malezi katika baadhi ya familia zetu za Kiislamu.

Kauli za matusi, lugha chafu na kukosekana kwa staha vilivyoonekana katika video zile, vinapaswa kuwa kengele ya tahadhari kwa wazazi. Haiwezekani kila tunapokutana na tabia zisizofaa kwa watoto wetu tukimbilie kulaumu mazingira, marafiki, mitandao ya kijamii au shule, bila kujiuliza sisi wenyewe tumetekeleza wajibu wetu kiasi gani.

Mtoto hakui kwa mavazi anayovaa pekee. Hawezi kuitwa mwenye maadili mema kwa sababu tu amevaa ushungi, kanzu, kofia au vazi jingine linalotambulika katika jamii ya Kiislamu. Maadili ya kweli huonekana katika maneno, matendo, heshima na namna mtu anavyowatendea wengine.

Hapa ndipo tunapopaswa kujitazama wazazi wa Kiislamu. Tumekuwa tukisisitiza watoto wetu wavae mavazi yanayokubalika kidini, lakini je, tunatumia nguvu hiyo hiyo kuwafundisha namna ya kuzungumza, kuheshimu watu, kujisitiri kimaadili na kujitambua wanapokuwa mbele ya jamii?

Kwa kweli, wahitimu wale wametuvua nguo sisi wazazi wa Kiislamu. Si kwa sababu tunapaswa kuwahukumu wote kuwa hawana maadili, bali kwa sababu tukio lao limetuonesha kuwa kuna pengo kubwa kati ya tunachotaka watoto wetu waonekane na kile tunachowafundisha kuwa.

Mzazi ni mchungaji

Katika Uislamu, malezi ya watoto si jambo la hiari wala jukumu linaloweza kukabidhiwa kwa walimu wa shule na madrasa pekee. Ni dhamana ambayo Mwenyezi Mungu amewapa wazazi na walezi.

Mtume Muhammad (Rehema na amani za Allah zimshukie) ameeleza jambo hili kwa msisitizo mkubwa kupitia hadithi mashuhuri iliyopokelewa na Imam Bukhari na Muslim.

Mtume anasema: “Kila mmoja wenu ni mchungaji na kila mmoja wenu ataulizwa kuhusu alichokichunga.”

Katika hadithi hiyo, Mtume anaeleza kuwa kiongozi ni mchungaji wa raia wake, mwanamume ni mchungaji wa familia yake, mwanamke ni mchungaji wa nyumba ya mume wake na watoto wake, na kila mmoja atawajibika kwa kile alichokabidhiwa.

Ujumbe wa hadithi hii ni mzito. Mzazi hawezi kujivua wajibu wa malezi kwa sababu mtoto ameanza kwenda shule, ameingia sekondari au amefikisha umri wa kujitegemea. Wajibu wa kumwelekeza, kumshauri na kumfundisha mema unaendelea.

Changamoto kubwa katika familia nyingi za sasa ni wazazi kuwa karibu na watoto kimwili, lakini mbali nao katika malezi. Wapo wanaojua watoto wao wanasoma shule gani, wanafanya mitihani lini na wanahitaji fedha kiasi gani, lakini hawajui marafiki zao, wanachofuatilia mitandaoni, lugha wanayotumia au changamoto zinazowakabili.

Wengine wameiachia shule kazi ya kufundisha kila kitu, madrasa ifundishe dini, huku nyumbani kukiwa hakuna utaratibu wa kuzungumza na watoto kuhusu mwenendo na wajibu wao katika jamii.

Hili ni kosa kubwa. Shule inaweza kumfundisha mtoto kusoma na kuandika, madrasa ikamfundisha kuswali na kusoma Qurani, lakini msingi wa tabia na mwenendo wake unapaswa kujengwa kwa kiasi kikubwa nyumbani.

Jambo jingine muhimu ni kutambua kuwa malezi si adhabu pekee. Ni mazungumzo, ushauri, upendo, kuweka mipaka na kusimamia utekelezaji wake. Mtoto anapokosea, mzazi ana wajibu wa kumrekebisha na kumweleza madhara ya tabia yake.

Kwa hiyo, tukio la wahitimu hawa lisiwe sababu ya kuwashambulia vijana au kuwahukumu kwa mavazi yao. Liwe nafasi ya wazazi wa Kiislamu kujitathmini na kurejea katika wajibu wao wa malezi.

Tukumbuke kuwa ushungi hauwezi kuchukua nafasi ya tabia njema, kama ambavyo mavazi mengine ya Kiislamu hayawezi kuwa mbadala wa uchamungu.

Tukubali tu kuwa wahitimu wale wametuvua nguo wazazi wa Kiislamu. Hivyo sasa ni wakati wa kuzivaa tena kwa kurekebisha malezi yetu. Tusisubiri watoto wetu wafanye jambo litakalotuaibisha mbele ya jamii ndipo tuanze kujiuliza tulikosea wapi.

خطبة الجمعة

IMEANDALIWA
Na Barnabas Mkwayu
0766 364 354

MIMBARI ZETU

KUTOKA

Masjid Al-Haram **(Makka)**

Masjid Nabawi **(Madina)**



MIMBARI ZETU

خطبة الجمعة

MSIKITI MTAKATIFU, MAKKA

IMAMU NA KHATIBU SHEIKH DKT. SALEH BIN ABDULLAH BIN HUMAID



Imamu Makka ataja siri 3 za kupata utulivu wa moyo

MAKKA, Saudi Arabia — Imamu na Khatibu wa Msikiti Mkuu wa Makka, Sheikh Dkt. Saleh bin Abdullah bin Humaid, amesema utulivu wa kweli wa moyo na furaha ya maisha havitegemei wingi wa mali, bali uimara wa imani, kumtegemea Allah na kuridhika na maamuzi Yake.

Katika khutba ya Ijumaa, Oktoba 23, 2026, Sheikh Bin Humaid alisema baadhi ya watu huishi kwa utulivu na kuridhika licha ya changamoto zinazowakabili, huku wengine wakiwa na mali na starehe nyingi lakini wakiendelea kukabiliwa na huzuni, wasiwasi na kutoridhika.

Alieleza kuwa tofauti hiyo inahusiana na kile kinachoitwa halawatuliman, yaani utamu wa imani, ambao humwezesha muumini kupata utulivu wa ndani na kustahimili misukosuko ya maisha.

Kwa mujibu wa khatibu huyo, utamu wa imani hupatikana kwa kuridhika na Allah kuwa Mola, Uislamu kuwa dini na Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) kuwa Mtume na Mjumbe wa Allah. Alisema kuridhika na Allah kunamaanisha kutambua kuwa Yeye ndiye Muumba, Mruzuku na Msimamizi wa mambo yote, huku kuridhika na Uislamu kukimaanisha kuukubali kama mwongozo wa maisha; na kuridhika na Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) kunamtaka Muislamu kufuata mafundisho, mwenendo na Sunna zake. Sheikh Bin Humaid alisema Muumini mwenye imani thabiti hushukuru anapopewa neema, huwa na subira anapokosa anachokitamani na hukimbilia kutubu anapofanya dhambi.


Alionya kuwa kudhoofika kwa imani kunaweza kumfanya mtu kuwa mwenye wasiwasi, kukata tamaa na kutawaliwa na ubinafsi, hali inayoweza kuathiri pia uhusiano wake na wengine.

Aliwahimiza Waislamu kuimarisha uchamungu, kufanya ibada kwa ikhlasi, kushikamana na Sunna na kujitahidi kutenda mema.

Alisisitiza kuwa furaha ya kweli inapaswa kutafutwa katika uhusiano wa mtu na Allah, badala ya kutegemea mafanikio ya mali na starehe za dunia pekee.

MSIKITI WA MTUME, MADINA

IMAM NA KHATIBU SHEIKH DKT. ALI BIN ABDULRAHMAN AL-HUDHAIFI



Umoja wa Waislamu ujengwe katika Tauhidi, Qur'an na Sunna

MADINA, Saudi Arabia — Imamu na Khatibu wa Msikiti wa Mtume mjini Madina, Sheikh Dkt. Ali bin Abdulrahman Al-Hudhaifi, amewataka Waislamu kuimarisha umoja wao kwa kushikamana na Tauhidi, Qur'an na Sunna, akisisitiza kuwa kutamka shahada mbili pekee hakutoshi bila kuzitekeleza katika maisha.

Katika khutba ya Ijumaa, Oktoba 23, 2026, Sheikh Al-Hudhaifi alisema shahada ya kushuhudia kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na kwamba Muhammad ni Mtume Wake ndiyo msingi wa imani ya Kiislamu.

Alieleza kuwa shahada ya kwanza inamtaka Muislamu kuelekeza ibada zote kwa Allah pekee, bila kumshirikisha na chochote, huku shahada ya pili ikimtaka kumtii Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani), kuamini aliyoyafundisha na kufuata Sunna zake.

Khatibu huyo alisema Waislamu wanapaswa kuungana katika matendo kama walivyoungana katika kutamka shahada hizo, kwa kuimarisha udugu, kusaidiana na kuepuka mifarakano.

Akizungumzia umuhimu wa Tauhidi, Sheikh Al-Hudhaifi alisema ujumbe wa msingi wa Mitume wote ulikuwa kuwaelekeza watu kumwabudu Allah pekee na kujiepusha na shirki.

Alisisitiza pia umuhimu wa kumtambua Allah kupitia Majina na Sifa Zake zilizotajwa katika Qur'an na Sunna, kwa kufuata mafundisho ya Mtume na Maswahaba zake.

Kwa mujibu wa khatibu huyo, Waislamu wana mambo muhimu yanayowaunganisha, yakiwamo itikadi, lugha ya Kiarabu inayotumika katika ibada, historia ya ujumbe wa Mitume na Kibla kimoja.

Alitumia aya ya 103 ya Suratu Aal Imran inayowaamrisha Waumini kushikamana na kamba ya Allah kwa pamoja na kutofarakana.

Sheikh Al-Hudhaifi alisema changamoto zinazowakabili Waislamu zinahitaji ushirikiano, kusaidiana na kuhurumiana, badala ya mifarakano inayodhoofisha nguvu za Umma.

٣٠
جُمَادَى الأُولَى
١٤٤٨ هـ

KUTOKA KWA MHARIRI

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
0789 201383

Wito wa viongozi wa Kikristo kuhusu Qur'an uzingatiwe

Tumefurahishwa na kauli za viongozi wa dini ya Kikristo nchini walioeleza kuwa kuifahamu Qur'an ni mojawapo ya njia muhimu za kuondoa propaganda, hofu na dhana potofu kuhusu Uislamu.

Viongozi hao walitoa kauli hiyo wakati wa maadhimisho ya miaka 70 ya Usajili wa Jumuiya za Kiraia yaliyofanyika wiki iliyopita katika Ukumbi wa Mlimani City, jijini Dar es Salaam.

Katika maadhimisho hayo, taasisi ya The Islamic Foundation iligawa nakala za tafsiri ya Qur'an kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza, pamoja na Juzuu Amma kwa washiriki mbalimbali wakiwamo wachungaji na maaskofu, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kueneza elimu ya Uislamu na kuongeza uelewa wa jamii kuhusu mafundisho yake.

Akizungumzia hatua hiyo, Askofu Andrew Wagana, alisema kitendo cha The Islamic Foundation kugawa nakala za tafsiri ya Qur'an bila malipo kinaonesha umuhimu wa kupanua uelewa kuhusu dini mbalimbali kupitia utoaji wa maarifa na vitendo vya ukarimu.

Kwa upande wake, Askofu Asher Agostino, alisema vitabu hivyo vitawawezesha watu wengi kuelewa ujumbe wa Qur'an na kuwashirikisha wengine maarifa watakayoyapata.

"Tukifahamu yaliyomo ndani ya vitabu hivi, itatusaidia kuwa mabalozi kwa wenzetu na kuwaeleza kile tulichokisoma, hivyo kuondoa dhana potofu na kuujua Uislamu wa kweli kupitia mafundisho yake," alisema Askofu Asher.

Sisi, gazeti la Imaan, tunaipongeza The Islamic Foundation kwa hatua hiyo, ambayo tunaamini ni mfano mzuri unaopaswa kuigwa na taasisi nyingine za dini.

Kugawa vitabu vya dini bila malipo si tendo la ukarimu pekee, bali pia ni uwekezaji katika elimu, maelewano na kuimarisha uhusiano mwema katika jamii. Jambo hili lina msingi wake katika mafundisho ya Qur'an.

Katika Sura ya Al–Ankabut (Qur'an, 29:46), Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "...wala msijadiliane na Watu wa Kitabu ila kwa njia nzuri zaidi, isipokuwa wale waliodhulumu miongoni mwao. Na semeni: Tumeamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwenu..."

Aya hii inatukumbusha umuhimu wa kuendesha mazungumzo baina ya watu wa imani tofauti kwa hekima, staha na kuheshimiana.

Kwa msingi huo, kujifunza kuhusu dini nyingine hakupaswi kuonekana kuwa tishio kwa imani ya mtu, bali ni fursa ya kuelewa misingi ya imani za wengine, kuondoa hofu, chuki na kupinga dhana potofu zinazoweza kusababisha uhasama baina ya waumini wa dini tofauti.

Mtu anayemfahamu mwenzake huwa na nafasi nzuri zaidi ya kufanya naye mazungumzo yenye tija kuliko yule anayejenga mtazamo wake kwa kutegemea taarifa zisizothibitishwa na dhana potofu.

Hata hivyo, juhudi za kuimarisha uhusiano mwema baina ya waumini wa dini mbalimbali hazipaswi kuachiwa taasisi ya The Islamic Foundation pekee. Taasisi nyingine za Kiislamu, viongozi wa dini na jumuiya za kiraia zinapaswa kushirikiana katika juhudi hizo ili kuimarisha umoja, mshikamano na amani nchini.

Kadhalika, wito wa viongozi wa Kikristo wa kuhamasisha uelewa kuhusu mafundisho ya Qur'an haupaswi kuishia katika maadhimisho ya miaka 70 ya Usajili wa Jumuiya za Kiraia, bali unapaswa kuendelezwa kupitia utamaduni wa kusoma, kuelewa na kuheshimu maandiko ya dini mbalimbali.

Juhudi hizo zitasaidia kuondoa dhana potofu, kuimarisha upendo, kuheshimiana, na kudumisha amani, uvumilivu na mshikamano katika jamii.

٣٠ جُمَادَى الأُولَى ١٤٤٨ هـ

NASAHA ZA WIKI

NA
Yusufu Amini
0787 503 085



Adhkar zina faida nyingi kwenye maisha yako

Dhikri ni ibada rahisi inayoweza kufanywa wakati wowote na mahali popote bila kuhitaji mali wala mazingira maalum. Pamoja na urahisi wake, ibada hii ina malipo makubwa na nafasi muhimu katika maisha ya kila siku ya Muislamu.

Hivyo, ni muhimu kuifanya kuwa sehemu ya maisha yetu ya kila siku badala ya kuikumbuka wakati wa matatizo pekee. Allah ametufundisha kumkumbuka na kumshukuru tunapotumia vyombo vya usafiri, iwe ni gari, ndege, meli au chombo kingine.

Katika Sura ya Az–Zukhruf (Qur'an, 43:13), Allah Mtukufu anasema: "...kumbukeni neema za Mola wenu Mlezi mnapokaa sawa sawa juu yao na mseme: Ametakasika aliyemfanya huyu atutumikie, na tusingeweza kuyafanya haya wenyewe."

Aya inayofuata, ya 14, inatukumbusha kuwa sote tutarejea kwa Mola wetu. Aya hizi zinatuhimiza kutambua neema ya usafiri na kutomtegemea binadamu au uwezo wa chombo pekee, bali kumtegemea Allah katika safari zetu.

Aidha, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) ametufundisha dua za safari za kumuomba Allah atuepushe na madhara, atulinde tunapokuwa mbali na familia zetu na aturudishe salama.

Dhikri katika biashara

Muislamu anapaswa kuhakikisha kuwa shughuli za kibiashara na kutafuta riziki hazimfanyi kumsahau Allah. Kutafuta mali ni jambo linaloruhusiwa katika Uislamu, lakini halipaswi kutangulizwa mbele ya ibada na wajibu wa kidini.

Katika Sura ya Al–Jumu'ah (Qur'an, 62:10), Allah anawaelekeza Waumini kuwa baada ya kumaliza sala ya Ijumaa watawanyike katika ardhi kutafuta fadhila zake huku wakiendelea kumkumbuka kwa wingi ili wafanikiwe.

Kwa hiyo, Muislamu anaweza kujishughulisha na biashara, ajira na shughuli nyingine za kiuchumi huku akiendelea kumkumbuka Mola wake. Jambo la msingi ni kuweka uwiano kati ya kutafuta riziki na kutekeleza wajibu wa kidini.

Dhikri ni kinga dhidi ya shari

Miongoni mwa faida za dhikri ni kupata ulinzi wa Allah dhidi ya shari za viumbe na madhara mbalimbali. Mtume amewahimiza Waumini kudumisha adhkari za asubuhi na jioni, zikiwamo dua za kuomba ulinzi wa Allah.

Miongoni mwa dua hizo ni: "Bismillaahi lladhii laa yadhurru ma'asmihi shay'un fil–ardhwi wala fis–samaa'i wahuwas–samii'ul–aliim." Maana yake: "Kwa jina la Allah ambaye kwa jina lake hakuna chochote kinachoweza kudhuru ardhini wala mbinguni, naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua."

Ni muhimu kufahamu kuwa kumtegemea Allah hakumaanishi kuacha kuchukua tahadhari au kutumia njia halali za kujikinga dhidi ya madhara.

Dhikri hutuliza moyo

Faida nyingine muhimu ya dhikri ni kuleta utulivu wa moyo. Allah anasema: "Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndiyo nyoyo hutulia." [Qur'an, 13:28].

Katika maisha ya sasa, watu wengi wanakabiliwa na changamoto za kifamilia, kikazi na kiuchumi. Hata hivyo, kwa kumkumbuka Allah, Muislamu anaweza kuwa na subira na kutambua kuwa kila jambo hutokea kwa uamuzi wake.

Ni njia ya kupata thawabu

Dhikri pia ni njia nyepesi ya kujipatia thawabu nyingi. Jambo la kuvutia ni kwamba baadhi ya dhikri ni nyepesi kutamka, lakini zina malipo makubwa mbele ya Allah.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Maneno mawili ni mepesi katika ulimi, mazito katika mizani na yanapendwa na Mwingi wa rehema: 'Subhanallahi wa bihamdihi, Subhanallahil – Adhwiim.'" [Bukhari na Muslim].

Hadith hii inaonesha ukubwa wa fadhila za dhikri. Muislamu anaweza kumtaja Allah akiwa nyumbani, kazini au safarini. Jambo la msingi ni kuwa na Ikhlas na kutambua maana ya maneno anayoyatamka.

٣٠ جُمَادَى الأُولَى ١٤٤٨ هـ

SAFARI YA MABADILIKO



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

ELIMU YA MAZISHI YA KIISLAMU

Baada ya mazishi: Ta'ziyah, kuwafariji wafiwa na adabu za msiba

SEHEMU YA **12**

Mara nyingi watu hufikiri kwamba wajibu kwa marehemu unaishia pale kaburi linapofunikwa kwa udongo. Lakini Uislamu umeangalia pia hali ya wale waliobaki nyuma: wazazi, watoto, wenzi wa ndoa na ndugu wa marehemu.
Baada ya mazishi, familia huingia katika kipindi kigumu cha huzuni, upweke na wakati mwingine changamoto za maisha. Ndiyo maana Uislamu umehimiza Waislamu wengine kusimama pamoja nao kwa faraja, dua na msaada. Hii inaitwa ta'ziyah.

Maana ya Ta'ziyah

Ta'ziyah ni kumfariji mwenye msiba, kumtia moyo awe na subira, kumkumbusha malipo ya Allah na kumuombea marehemu. Si lazima iwe hotuba ndefu au maneno mengi. Wakati mwingine maneno machache yenye ukweli na huruma yanaweza kuwa msaada mkubwa kwa mwenye huzuni.

Miongoni mwa dua zilizofundishwa ni: "Hakika ni vya Allah alivyovichukua, na ni Vyake alivyovitoa. Na kila kitu Kwake kina muda maalumu. Basi vumilia na tarajia malipo kutoka kwa Allah." [Hadith].

Lengo la kuwafariji wafiwa

Mosi, Ta'ziyah inalenga kuwakumbusha wafiwa umuhimu wa subira kwa sababu kifo ni sehemu ya qadar ya Allah.

Allah Mtukufu amesema: "Na kwa hakika Tutakujaribuni kwa kitu cha hofu, njaa, upungufu wa mali, nafsi na matunda. Na wape habari njema wenye kusubiri." [Qur'an, 2: 155). Mwenye msiba anahitaji kukumbushwa kwamba subira yake mbele ya Allah ina malipo.

Pili, Ta'ziyah inalenga kupunguza mzigo wa familia. Katika siku za mwanzo baada ya kifo, familia huwa na mambo mengi ya kushughulikia. Ndiyo maana Uislamu umehimiza majirani na ndugu kuwasaidia.

Chakula kwa wafiwa

Miongoni mwa Sunna nzuri ni kuandaliwa chakula kwa ajili ya familia ya marehemu.

Baada ya kufariki Ja'far bin Abi Twalib (Allah amridhie), Mtume (Allah amshushie rehema na amani) aliwaambia Swahaba: "Waandalieni familia ya Ja'far chakula, kwani wamepatwa na jambo litakalowashughulisha." [Abu Daud na Tirmidhi].

Hadith hii inaonesha hekima kubwa ya Kiislamu, kwamba, familia iliyofikwa na msiba inahitaji kusaidiwa, si kuongezewa majukumu.

Tatizo la kuwalazimisha wafiwa kupika

Katika baadhi ya jamii, jambo limegeuka kinyume chake. Badala ya watu kupeleka chakula kwa wafiwa, wafiwa wenyewe hujikuta wanapaswa kupika kwa ajili ya wageni wengi, kugharamia mikusanyiko, kukopa fedha kwa ajili ya msiba na kuhudumia wageni wakati wao wenyewe wana huzuni.

Hali hii inapingana na hekima ya Sunna kwani hakika mtu aliyefiwa anahitaji faraja, si mzigo mwingine.

Kulia kwa marehemu

Uislamu haujakataza machozi wala huzuni. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) mwenyewe alilia alipofariki mwanawe Ibrahim.

Mtume alisema: "Macho yanatoa machozi, na moyo unahuzunika, lakini hatusemi isipokuwa yanayomridhisha Mola wetu." [Bukhari].

Hii inaonesha mizani ya Uislamu, kwamba, huzuni ni ya kibinadamu, machozi yanaruhusiwa lakini mayowe, kujipiga na maneno ya kupinga qadar ya Allah hayaruhusiwi.

Kukaa kwa maombolezo

Baadhi ya jamii zina desturi ya kukaa kwa siku maalumu baada ya msiba. Katika suala hili, wanazuoni wametofautisha kati ya kukaa kwa ajili ya kuwapokea wanaokuja kutoa pole na kuifanya siku maalumu kuwa ibada yenye fadhila maalumu bila dalili.

Jambo la msingi ni kwamba Uislamu umehimiza faraja na msaada, lakini haujaweka sherehe maalumu za maombolezo baada ya kifo.

Mambo yanayopaswa kuepukwa

Baadhi ya mambo yanayoonekana katika jamii ni kuwalazimisha wafiwa kufanya mikusanyiko mikubwa, kushindana katika ukubwa wa chakula na kuingia kwenye madeni kwa ajili ya kuonesha heshima.

Mengine yanayopaswa kuepukwa ni kufanya msiba kuwa sehemu ya sifa na kujionesha na kusahau kumuombea marehemu kwa sababu ya shughuli nyingi.

Funzo kubwa na hitimisho


Muislamu aliyefariki anahitaji zaidi dua kuliko sherehe. Familia yake inahitaji zaidi faraja kuliko mashindano. Hivyo basi, majirani wanapaswa kuwa msaada, si mzigo. Hii ndiyo roho ya Uislamu katika kushughulikia msiba.

Nihitimishe kwa kusema kuwa Ta'ziyah ni ibada ya huruma.

Mtu anayemfariji mwenzake wakati wa msiba humsaidia kubeba maumivu yake, na hujenga mshikamano katika jamii ya Waislamu.

Tujifunze kutoka kwa Sunna ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani) wakati wa msiba, tusiongeze mzigo kwa waliofiwa; tuwapunguzie.

Makala ijayo: "Chakula katika Misiba: Sunna ya kuwasaidia wafiwa na marekebisho ya baadhi ya desturi."



Na Aunt Samrath
0789 201 383

Watoto, mnajua Allah anatuona kila wakati?

Assalamu alaikum, watoto wangu!

Leo Aunt Samrath ana hadithi nzuri sana!

Ni hadithi ya Mtume wetu Muhammad (Allah amshushie rehema na amani)na mgeni mmoja wa ajabu.

Hebu tulieni vizuri, mnisikilize!

Mgeni wa ajabu

Siku moja, Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) alikuwa amekaa pamoja na Maswahaba zake.

Ghafla, akatokea mwanaume mmoja!

Aliyekuwa amevaa nguo nyeupe pee. Nywele zake zilikuwa nyeusi tii. Hakuwa na vumbi wala dalili za safari.

Lakini cha kushangaza, hakuna aliyemfahamu!

Mgeni huyo akaketi karibu na Mtume (Allah amshushie rehema na amani)na kuanza kumuuliza maswali.

“Ewe Muhammad, nieleze kuhusu Uislamu.”

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) akamweleza kuhusu kumwamini Allah kuwa ndiye Muabudiwa pekee wa haki na Muhammad ni Mtume Wake, kuswali, kutoa Zaka, kufunga Ramadhani na kwenda Hijja kwa mwenye uwezo.

Mgeni akasema, “Umesema kweli!”

Maswahaba wakashangaa! Anauliza swali, halafu mwenyewe anasema jibu ni sahihi!

Akauliza tena kuhusu Imani.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) akamweleza kuhusu kumwamini Allah, Malaika, Vitabu Vyake, Mitume, Siku ya Mwisho na Qadar, yaani makadirio ya Allah.

Kisha mgeni akauliza swali jingine muhimu sana.

“Ewe Muhammad, nieleze kuhusu Ihsan.”

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) akajibu:

“Ni kumwabudu Allah kana kwamba unamuona. Na ikiwa humuoni, basi Yeye anakuona.”

Baadaye, mgeni huyo akaondoka.

Mtume akawauliza: Maswahaba zake. Mnamjua yule aliyekuwa anauliza maswali alikuwa nani?

Wakasema: Allah na Mtume wake ndiye wamjuwae zaidi.

Mtume akawaambia: Yule alikuwa Malaika Jibril (amani juu yake)! Allah alimtuma kuja kuwafundisha watu dini yao.

Ihsan ni nini?

Watoto wangu,

Aunt Samrath anataka mjifunze neno moja leo: IHSAN!

Ihsan maana yake ni kufanya mambo mazuri kwa moyo wa kweli, tukikumbuka kuwa Allah anatuona.

Hebu fikirieni!

Mama amekuachia pipi mezani na kukuambia usizile mpaka arudi

Mama akiondoka, unajua hakuna mtu anayekuona.

Utazila Hapana!

Kwa nini? Kwa sababu Allah anakuona.

Na unataka kuwa mtoto mwaminifu.

Au unamkuta mtoto mwenzako ameangusha penseli yake.

Unaweza kuichukua bila mtu kujua.

Lakini unamrudishia!

Kwa nini? Kwa sababu Allah anapenda uaminifu.

Tunawezaje kufanya Ihsan?

Watoto wangu, mnaweza kufanya Ihsan kila siku!

Mnaposwali, swalini vizuri kwa ajili ya Allah.

Mnaposoma Qur’an, someni kwa makini.

Mnapowasaidia Mama na Baba, fanyeni hivyo kwa furaha.

Mnapokosea, ombeni msamaha na mjitahidi kutorudia.

Na hata mnapokuwa peke yenu, chagueni kufanya mema.

Kumbukeni, Allah anajua hata jambo zuri dogo mnalolifanya!

Swali la Aunt Samrath!

Sasa, watoto wangu, nani anaweza kuniambia:

Mtu anayetenda mema kwa ajili ya Allah, hata bila kuonekana na watu, anafanya nini?

Ndiyooo! Anafanya Ihsan!

Na mtu anayejitahidi kufanya Ihsan anaitwa Muhsin.

Aunt Samrath anatamani wote muwe watoto wema, waaminifu na wenye kumpenda Allah.

Kumbukeni: Hata kama hakuna mtu anayekuona ukifanya jambo zuri, Allah anakuona!

Hadi tutakapokutana tena, watoto wangu!

Assalamu alaikum!

NA
Na Said Rajab
0783 650 803

Matumizi ya Akili Unde kwa mtazamo wa Kiislamu



Katika sehemu iliyopita ya makala haya, tulieleza kuwa wasanifu wa programu za Akili Unde (AI) wana wajibu wa kulinda faragha za watumiaji kwa kuzingatia kanuni ya Kiislamu ya Sitr, inayosisitiza umuhimu wa kuhifadhi siri na kulinda faragha za watu. Aidha, tuliwasisitiza wataalamu hao kuhakikisha kuwa mifumo ya AI haibagui wala kusababisha madhara kwa jamii za Waislamu. Vilevile, tuliwataka wabuni zana za AI zinazohudumia Umma, kuendeleza elimu ya Kiislamu, kuboresha huduma za afya na kuchochea maendeleo ya kiuchumi. Katika sehemu hii ya tano na ya mwisho, tutaangazia namna bora ya Waislamu kutumia Akili Unde na kuepuka matumizi yake mabaya.

Waislamu wanapaswa kutumia AI kwa kubuni programu tumizi (Apps) za kujifunza Qur'an, kutafuta hadith za Mtume (rehema na amani ya Allah zimshukie) na kuvumbua maarifa ya Uislamu.

Aidha, wanapaswa kutumia AI kukagua na kuboresha kazi zao na siyo kupuuza juhudi zao za kujifunza. Ni muhimu kuelewa matokeo yanayotolewa na AI badala ya kuyanakili moja kwa moja.

Vilevile, taarifa na maudhui ya kidini yanayozalishwa na AI yanapaswa kuthibitishwa mara kwa mara na wanazuoni wenye ujuzi wa masuala ya Kiislamu ili kuepuka kusambaza taarifa zisizo sahihi.

Waislamu wanapaswa pia kusoma na kuelewa sera za faragha za zana za AI wanazotumia ili kulinda taarifa zao binafsi. Aidha, wanapaswa kutumia AI kwa tija katika shughuli halali za biashara, utafiti na usaidizi wa uandishi.

Pamoja na hayo, ni muhimu kuwa waangalifu katika matumizi ya muda. Mitandao ya kijamii inayotumia teknolojia ya AI imeundwa kwa namna inayoweza kuwafanya watumiaji kutumia muda mwingi zaidi kuliko walivyokusudia.

Kwa hiyo, Waislamu wanapaswa kutumia muda wao kwa busara na kuhakikisha kuwa matumizi ya teknolojia hayaingilii majukumu yao ya kidini, hususan utekelezaji wa ibada ya sala kwa wakati.

Epuka matumizi haya ya AI

Usikubali fat–wa au hukumu yoyote ya kidini inayotolewa na AI bila kwanza kuithibitisha kwa wanazuoni wenye ujuzi wa masuala ya Kiislamu. Vilevile, unapaswa kuepuka kutumia AI kutengeneza maudhui ya udanganyifu, picha au sauti bandia, na kusambaza taarifa potofu.

Aidha, si sahihi kuwasilisha kazi zilizotengenezwa kwa kutumia Akili Unde katika mazingira ya elimu au taaluma kana kwamba ni kazi zako binafsi, bila kuweka wazi mchango wa teknolojia hiyo. Kitendo hicho kinakinzana na maadili ya Kiislamu yanayosisitiza ukweli, uaminifu na uadilifu.

Kamwe usiruhusu mifumo ya AI ikuamulie maudhui ya Kiislamu unayotumia. Badala yake, hakikisha unatafuta na kutumia vyanzo vya kuaminika. Usichukulie AI kuwa teknolojia isiyoweza kukosea, kwani inaweza kutoa taarifa zisizo sahihi, kuwa na upendeleo na hata kuwapotosha watumiaji.

٣٠ جُمَادَى الأُولَى ١٤٤٨ هـ

Na Said Rajab
0783 650 803

KIMATIFA

SEHEMU YA MWISHO 4

Miaka mitatu ya mateso Gaza, nini kifanyike?



Wiki iliyopita, tulihitimisha kwa kueleza kuwa mgogoro wa Gaza si suala la kibinadamu au kisiasa pekee, bali pia unahusu uvamizi wa kijeshi katika ardhi iliyobarikiwa. Kwa msingi huo, tulieleza kuwa suluhisho la mgogoro huo liko mikononi mwa majeshi ya umma wa Waislamu duniani kote.

Tulisisitiza kuwa uvamizi wa kijeshi unahitaji jibu la kijeshi, na kwamba hilo ni takwa la kisharia na ulazima unaokubalika na akili timamu. Katika sehemu hii ya mwisho, tutaangazia umuhimu wa kuchukua hatua sahihi na halali katika kufikia ushindi unaotafutwa, kwa kuzingatia kuwa ushindi hutoka kwa Allah. Aidha, tutajadili umuhimu wa mshikamano na juhudi za pamoja za Waislamu duniani katika kuikomboa Palestina, kwa kuzingatia misingi ya sheria, haki na amani.

Msimamo imara kwa Palestina

Umma wa Waislamu unapoamka, unapaswa kudumisha msimamo thabiti bila kuyumba, kufanya makubaliano au kurudia hatua zilezile zinazopendekezwa na mataifa ya Magharibi, ambazo kimsingi zinaendeleza mateso ya Wapalestina na kuwalinda wahalifu wa Kizayuni.

Allah anasema: “Wala msilegee wala msihuzunike, ilihali nyinyi ni waumini wa kweli na mko juu.” [Qur’an, 3:139]. Wajibu wetu kama Waislamu si kupinga tu ukandamizaji dhidi ya Wapalestina, bali pia kuunga mkono juhudi za kutafuta suluhisho la haki na la kudumu katika mgogoro wa Palestina.

Hatua hii inahitaji zaidi ya maandamano au mazungumzo ya amani. Inahitaji kusimamishwa kwa Uislamu na kuratibiwa kwa uhamasishaji wa majeshi ya Waislamu kutoka sehemu mbalimbali za dunia.

Katika mazingira haya, wajibu wetu ni kueneza uelewa sahihi wa Uislamu, kushiriki katika hatua za kijamii zilizopangwa, na kuunganisha mateso yanayoendelea Gaza na mradi mpana wa kufufua mfumo wa haki wa Kiislamu.

Uimara wa wananchi wa Gaza unatoa ujumbe mzito kwa Waislamu duniani. Hatuwezi kuendelea kuwa watazamaji wa yanayoendelea; tunapaswa kuonesha mshikamano na kupinga dhuluma kwa njia za amani na kisheria, kwani vita hii haiwahusu wakazi wa Gaza pekee, bali inatuhusu sote.

Gaza ni kioo cha umma wetu. Magofu yake yanaonesha udhaifu wetu, huku uimara wake ukidhihirisha uwezo wetu. Hali ya yatima wake inaamsha dhamiri zetu, na ustahimilivu wa wananchi wake unathibitisha kuwa njaa na vikwazo haviwezi kuzima mwanga wa imani.

Allah Ta’ala anasema katika Qur’an: “Na Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya Makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya Makhalifa waliokuwa kabla yao. Na bila shaka atawasimamishia Dini yao aliyowapendelea, na kwa yakini atawabadilishia amani baada ya hofu yao, wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na watakaokufuru baada ya hayo, basi hao ndio wapotovu.” [Qur’an, 24:55].

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494

٣٠ جُمَادَى الأُولَى ١٤٤٨ هـ



MAISHA YA MTUME AYUB NA KAUMU YAKE

SEHEMU YA 12

Msomaji wangu mpendwa utakumbuka kwamba, katika mfululizo wa makala zetu na kwa kupitia matoleo kadhaa, tulikuwa tukiwasilisha – kwa kadri ya uelewa wetu-simulizi ya Mtume Musa (amani ya Allah iwe juu yake) pamoja na kaumu yake (Wana wa Israil) kama zilivyopokelewa kutoka katika vitabu. Tuliona mapambano makali baina ya haki na batili. Haki iliyofungamana na Tawhid (kumpwekesha Allah) na sharia aliyokuja nayo Mtume Musa na nduguye Haruna, ambayo ilipata upinzani mkali wa jabari Fir-aun muovu na watu wake, lakini tulishuhudia ushindi mkubwa wa Mitume hao kupitia miujiza kadhaa ikiwemo fimbo aliyoitumia Nabii Musa dhidi ya wachawi na pale alipoipiga bahari ikapasuka Wana wa Israil wakapita salama katikakati na yakazamishwa majeshi ya Fir-aun.

Simulizi hizi ndani ya Qur'an zina lengo la kuwataka walimwengu waliokuja baadae kujifunza kupitia yaliyowakuta wenzao ili maisha yao yawe ya maana na wafikie malengo la kuumbwa kwao.

Allah Mtukufu anasema: " Kwa hakika simulizi zao (Mitume wa Allah na kaumu zao) ni mazingatio kwa wenye akili. Haikuwa (hii Qur'an) hadithi iliyozuliwa lakini ni kisadikishaji cha yale (mafunzo) yaliyotangulia (katika vitabu), na ufafanuzi wa kila kitu na uongofu na rehema kwa watu wenye kuamini." [Qur'an, 12:111].

Kwa upande mwengine, simulizi hizi zinatutaka tuamini kwamba, kuna nguvu kubwa isiyowezekana yenye hekima, uwezo, matakwa na vipawa vya juu vya elimu isiyo mipaka, ambayo itakalo ndilo huwa na ambayo ndio inayoyatawala maumbile na viumbe wakiwemo binadamu. Nguvu hiyo ni Allah Mtukufu Asiye na Mshirika na Asiye na afananaye naye katika dhati yake, sifa zake na matendo yake.

Nabii Ayub

Basi katika toleo hili tutaanza kuyaangazia maisha ya Mtume Ayub (amani ya Allah imshukie) ambaye simulizi yake katika Qur'an ni miongoni mwa visa vyenye msisimko mkali.

Simulizi hii ni kielelezo cha ukubwa wa neema za Mwenyezi Mungu juu ya waja wake Waumini wenye subra ya hali ya juu kwa mitihani na mabalaaa yanayowafika kutoka kwa Mola wao.

Mtindo wa Qur'an kwa kisa cha Nabii Ayub

Mtindo wa kisa au simulizi ya Mtume Ayub katika Qur'an unatofautiana kidogo na mtindo wa simulizi za Mitume wenzake.

Naam, katika simulizi nyingine za Mitume kama vile Nuh, Hud, Swaleh, Musa, Shuaib na wengineo tuliona ikisimuliwa jinsi kila Mtume alivyowafikishia ujumbe kaumu yake akiwaita katika kumuabudu Mola wao, nasaha na miongozo yake kwao, upinzani wao na hatimae kuadhibiwa.

Lakini kwa upande wa simulizi ya Nabii Ayub (amani ya Allah imshukie), aya sana sana zimeelezea majaribu (mtihani) yaliyomkuta hadi kupoteza neema alizokuwa nazo zikiwemo fedha, mashamba, mifugo, wake, wajakazi, wafanya kazi, afya nk.

Simulizi inaonesha subira aliyoionesha na hatimaye kurejeshewa tena neema hizo na hata kuzidishiwa maradufu, kama tutakavyoona inshaAllah.

Katika hadith tunasoma: "Watu wanaopewa mitihani mikubwa zaidi ni Mitume, kisha watu wema, kisha wanaofuatia kisha wanaofuatia." [Ibn Majah].

Na katika hadithi nyingine anasema: "Mtu hujaribiwa kwa kadri ya dini (Imani) yake. Ikiwa yuko imara katika dini yake, huongezewa mitihani." [Tirmidh na Ibn Majah].

VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

Jina na nasabu yake

Jina lake ni Ayub bin Mu'us bin Zarih bin Aisuu bin Is-haq bin Ibrahim [taz: Aysaru Tafaasiir j.3 uk.116]. Hivi ni kusema kwamba Nabii Ayub alitokana na kizazi cha Nabii Ibrahim kutokana na mwanawe Is-haq.

Qur'an inatusogeza kwenye ufahamu huo pale Allah aliposema: "...na katika kizazi chake (Ya'kub): Daud, na Suleiman, na Ayoub, na Yusuf, na Musa na Haruna, na hivi ndivyo tuwalipavyo wafanyao wema." [Qur'an, 5:84].

Si Qur'an wala Sunna ya Mtume iliyoweka wazi maeneo aliyoishi Mtume Ayub (amani ya Allah imshukie), licha yakuwa kuna baadhi ya wana historia kudai kwamba aliishi maeneo ya "Hawraan" kusini mwa Syria. Allah Ndiye Ajuwae.

Utajiri wa Mtume Ayub

Mtume Ayobu alikuwa tajiri mkubwa sana katika jamii yake. Alimiliki mashamba, mifugo pamoja na idadi kubwa ya watoto, wafanya kazi na watumwa. Pia alikuwa na afya njema.

Lakini, Allah alimjaribu mja wake huyo, na neema zote hizi zikamtoka. Isitoshe, akajaribiwa kwa maradhi katika mwili wake yaliyodumu kwa muda mrefu.

Inaelezwa kuwa hakijabakia kiungo chochote kizima katika mwili wake ila moyo na ulimi wake akimtaja Mola wake kwavyo.

Uvumilivu wake

Pamoja na balaa na mitihani hiyo, Mtume Ayub alivumilia huku akimshukuru Mola wake, akimtaja kwa wingi kwa moyo na ulimi wake. Mtume Ayub hakumlalamikia na kuonesha kushindwa na subra au kuwa na jaza-I (fazaiko) lolote. Alibaki katika hali ya maradhi kwa miaka kadhaa.

٣٠ جُمَادَى الأُولَى ١٤٤٨ هـ

TAFAKURI YA WIKI

NA SAMRATH MSUYA
0789 201 383

Hivi kweli tusubiri kuugua ndipo tujifunze umuhimu wa usafi?



Unafika kwenye banda la chipsi. Karai limewekwa kwenye moto mkali, lakini ukiangalia mafuta yaliyomo, unaogopa. Meusi! Humo ndimo vinamoingia viazi, kuku, mishikaki na kila kinachohitaji kukaangwa.

Mbele ya banda hilo kuna mfereji wa maji machafu. Maji yanatiririka yakitoa harufu mbaya. Nzi wanaruka kila upande. Wengine wanatua kwenye vyakula, kisha wanarudi mferijini kuendelea na shughuli zao.

Hiki ni kijiwe kimoja cha chipsi mitaa ya Mburahati, Dar es Salaam. Lakini nina hakika kila Mtanzania anayesoma makala hii anaweza kutaja angalau kijiwe kimoja chenye mazingira yanayofanana na haya.

Ukienda kwa mama ntilie, nako kuna vituko vyake.

Mama anahangaika kumnyonyesha mtoto, huku akiendelea kukata nyanya za kuandaa chakula. Mahali pengine vyombo vinaoshwa kwenye maji ambayo yametumika mara kadhaa, huku vyakula vikiwa wazi, vikisubiri wateja na nzi kwa pamoja.

Kwa muuza samaki, unaweza kukuta samaki wamepangwa kwenye meza kando ya barabara. Vumbi linapita, nzi wanatua na kuondoka. Muuzaji anawapangua na kuwapanga upya kwa mikono mitupu.

Muda mfupi uliopita, mikono hiyo hiyo imepokea noti chafu kutoka kwa mteja au jirani yake wa buchani.

Kwa muuza matunda nako si tofauti sana. Anakupasulia tunda, anakata vipande na kukukabidhi. Hakuna kunawa mikono kati ya kupokea fedha na kushika chakula.

Haya si matukio ya kubuni. Ni mazingira ambayo tumeyazoea kiasi kwamba hayatushtui tena.

Na hapo ndipo tatizo kubwa lilipo.

Uchafu umeanza kuwa jambo la kawaida.

Unapoona chakula kinaandaliwa karibu na maji taka na watu wananunua bila wasiwasi, unapaswa kujiuliza: Hivi tumefikia hatua gani katika uelewa wa usafi?

Si kila uchafu unaonekana kwa macho. Chakula kinaweza kuonekana kizuri, lakini kikawa kimechafuliwa na vijidudu vinavyoweza kusababisha magonjwa.

Mafuta yaliyotumika kupita kiasi, mikono michafu, vyombo visivyosafishwa vizuri na nzi wanaotua kwenye chakula ni mambo yanayopaswa kututia wasiwasi.

Cha kushangaza zaidi ni kwamba matatizo haya hayapo kwenye vibanda vya chakula pekee. Yanaweza kuwa kielelezo cha namna tunavyochukulia usafi katika maisha yetu ya kila siku.

Ikiwa jamii nzima inayaona mazingira haya na hakuna anayeshtuka, huenda viwango vyetu vya usafi hata majumbani vinahitaji kuangaliwa upya.

Hivi mabwana na mabibi afya wako wapi?

Swali hili halipaswi kuchukuliwa kama lawama kwa watumishi hao pekee. Lakini ni lazima tujiulize kazi ya elimu ya afya kwa jamii inafanyika kwa kiwango gani.

Miongoni mwa majukumu ya maafisa afya ya mazingira ni kuelimisha jamii kuhusu kinga ya magonjwa, kusimamia usafi wa chakula na maji, udhibiti wa taka na utekelezaji wa sheria za afya ya mazingira.

Sasa, kama haya ndiyo majukumu yao, kwa nini mazingira ya aina hii yanaendelea kuwa sehemu ya kawaida ya biashara zetu?

Je, tatizo ni uhaba wa watumishi? Ukosefu wa vifaa? Usimamizi hafifu? Au tumeelekeza nguvu nyingi kwenye ukaguzi na adhabu kuliko elimu inayobadilisha tabia?

Nadhani tunahitaji kampeni kubwa na endelevu ya elimu ya usafi. Si kampeni ya siku moja, wala operesheni inayokuja na kuondoka.

Tunahitaji elimu inayowafikia wauza chakula, wateja, wazazi, watoto na jamii nzima. Elimu inayomfanya mtu aone aibu kuuza chakula kwenye uchafu, na mteja aone hatari ya kununua chakula katika mazingira hayo.

٣٠ جُمَادَى الأُولَى ١٤٤٨ هـ

NA ZAHARANI BARAKA

MATUKIO YENYE MAZINGATIO

Makosa katika fat–wa na athari zake kwa jamii

Mtu mmoja alimwendea mwanazuoni mashuhuri, Al–Izz Ibn Abdus–Salaam, anayejulikana kwa jina la Sultani wa Wanazuoni na kumuuliza kuhusu jambo fulani. Al–Izz (Allah amrehemu) alimjibu kwa kutoa fat–wa, lakini mtu huyo alipoondoka aligundua kuwa fat–wa aliyokuwa ametoa ilikuwa na makosa.

Hata hivyo, hakung'ang'ania msimamo wake, bali alikiri kosa hilo bila kusita. Baadaye alimlipa mtu ili azunguke katika maeneo mbalimbali ya nchi na kutangaza: "Yeyote aliyemuuliza (Al–Izz) kuhusu jambo lolote, asifanyie kazi fat–wa aliyompa kwa kuwa ina makosa."

Kwa kufanya hivyo, Al–Izz alionesha kuwa heshima, cheo, elimu wala aibu ya kukiri kosa havipaswi kumzuia mtu kurejea kwenye ukweli. [Taz: 'Mausu'at al–akhlaq wazzuhd warraqaiq']

Mafundisho ya tukio

Katika zama hizi za teknolojia na mitandao ya kijamii, kila mtu ana nafasi ya kutoa maoni kuhusu masuala mbalimbali. Hata hivyo, hali inatia wasiwasi zaidi pale watu wanapozungumzia dini ya Allah bila kuwa na elimu sahihi.

Baadhi yao huthubutu kutoa fat–wa, kuhalalisha au kuharamisha mambo bila kurejea dalili na misingi ya kielimu. Historia ya Uislamu inatufundisha kuwa wanazuoni wema walikuwa na tahadhari kubwa wali-pozungumzia masuala ya dini.

Walipobaini kuwa wamekosea, hawakusita kukiri na kurekebisha makosa yao. Kutokana na mwenendo huo, tunapata mafunzo muhimu yafuatayo:

Mosi, kukiri kosa ni sehemu ya ujasiri

Kukiri kosa si udhaifu bali ni ishara ya ujasiri, ukomavu na uaminifu katika dini. Ujasiri haupimwi kwa uwezo wa kukabiliana na wengine pekee, bali pia kwa uwezo wa kuishinda nafsi, kukubali makosa na kusimamia ukweli.

Ikiwa wanazuoni wakubwa hawakusita kukiri makosa yao, kwa nini baadhi ya watu leo hutumia dini kujitafutia umaarufu kwa kutoa fat–wa zisizo na msingi na kusambaza taarifa zisizo sahihi.

Pili, ukweli ni muhimu kuliko heshima ya mtu

Al–Izz alikuwa mwanazuoni mashuhuri, lakini hakuruhusu cheo chake kimzuie kukiri kosa. Hii inatufundisha kuwa dalili na ukweli vinapaswa kutangulizwa kuliko misimamo ya watu. Kunyamazia kosa baada ya kulibaini ni kukiuka wajibu wa kusimamia haki.

Tatu, mwanazuoni anapaswa kurekebisha makosa yake

Makosa katika fat–wa yanaweza kuwaathiri watu wengi. Hivyo, mwanazuoni anapobaini kuwa amekosea anapaswa kurekebisha hukumu hiyo. Huu ni mwenendo unaopaswa kuigwa na wanazuoni, walimu na walinganiaji.

Nne, aibu isiwe kikwazo cha kurejea kwenye haki

Baadhi ya watu wenye vyeo na heshima katika jamii husita kukiri makosa kwa kuhofia kupoteza hadhi zao. Kimsingi, aibu haipaswi kuwa kisingizio cha kuukataa ukweli.

Muislamu anapaswa kuwa tayari kuacha msimamo wake pale ukweli unapomdhihirikia. Allah anasema: "Wala msichanganye haki na batili, wala msifiche ukweli hali ya kuwa mnaujua." [Qur'an, 2:42].

Aidha, Mtume (rehema na amani za Allah zimshukie) amesema: "Hakuna husuda inayofaa isipokuwa katika mambo mawili: Mtu ambaye Allah amempa mali, naye akaitumia katika haki; na mtu ambaye Allah amempa elimu, naye anahukumu kwa kutumia elimu hiyo na kuwafundisha wengine." [Bukhari na Muslim].

Imam Malik pia aliwahi kusema: "Kila mtu kauli yake inaweza kukubaliwa au kukataliwa, isipokuwa mwenye kaburi hili," akimaanisha Mtume Muhammad (rehema na amani zimshukie). Hii inathibitisha kuwa kipimo cha mwisho cha haki ni Qur'an na Sunna sahihi, si misimamo ya watu.

Ujumbe huu ni muhimu kwa walimu, maimamu, wanazuoni na walinganiaji. Mwalimu anapokosea akubali kurekebishwa; Imam anapobaini kosa katika hukumu yake arejee kwenye usahihi; na mwenye kutoa fat–wa anapogundua kuwa amekosea asisite kutangaza marekebisho.

Kuna tofauti kati ya mtu anayependa kuonekana kuwa sahihi na yule anayethamini ukweli. Wa kwanza hung'ang'ania kauli yake hata pale anapobaini kuwa amekosea, kwa sababu kwake kukiri kosa ni sawa na kukubali kushindwa.

Wa pili huwa tayari kubadili msimamo wake mara tu ukweli unapodhihirika, kwa sababu ukweli una thamani kubwa kwake kuliko kushikilia msimamo usio sahihi.

Allah anasema: "Sema: Hakika Mola wangu ameharamisha mambo machafu, yaliyo wazi na yaliyofichikana, na dhambi, na uadui bila haki, na kumshirikisha Allah na kile ambacho hakukiteremshia dalili yoyote, na kusema juu ya Allah yale msiyoyajua." [Qur'an, 7:33].

Katika aya nyingine Allah anasema: "Na miongoni mwa watu wapo wanaowapoteza wengine kutoka katika njia ya Allah bila elimu, na wanaifanya njia hiyo kuwa ni mzaha. Hao watapata adhabu yenye kudhalilisha." [Qur'an, 31:6].

Kwa hiyo, Muislamu anapaswa kuwa na tahadhari kabla ya kutoa hukumu kuhusu halali na haramu. Mtu anayejadili masuala ya dini bila elimu ya kutosha anaweza kuwapotosha wengine na hata kujipotosha mwenyewe, huku akichangia watu kuiacha haki na kupotea katika njia iliyo sahihi.

UONGOZI
UTAWALA

Na Ukhti Fatima SS
0789 201 383

Makosa 10 ya viongozi katika kushughulikia migogoro kazini

Meneja wa Ugavi na Afisa Utumishi wamezozana vikali kwenye kikao. Kilichoanza kama tofauti ya maoni kuhusu utendaji wa kazi kimegeuka kuwa matusi na vitisho. Wafanyakazi wengine wameshuhudia tukio hilo, huku baadhi wakianza kuunga mkono upande mmoja. Wewe, ukiwa mkuu wao, umeamua kukaa kimya. Unaamini hasira zitapoa na wawili hao watasuluhisha tofauti zao wenyewe.

Huenda unakosea.

Mgogoro huo unaweza kuendelea kimya-kimya, ukazalisha makundi kazini, ukaharibu ushirikiano na hatimaye kuathiri utendaji wa taasisi nzima.

Hili ni mojawapo ya makosa yanayofanywa na viongozi wanaposhughulikia migogoro kazini.

Migogoro yenyewe si jambo baya kila wakati. Wafanyakazi wanaweza kutofautiana kuhusu mawazo, vipaumbele au namna ya kutekeleza majukumu. Tofauti hizo zikisimamiwa vizuri zinaweza kuzaa ubunifu na maamuzi bora.

Tatizo huanza pale viongozi wanaposhindwa kutambua tofauti kati ya mjadala wenye tija na mgogoro unaoharibu mahusiano.

Mbali na kukaa kimya, yapo makosa mengine tisa ambayo viongozi wanapaswa kuyaepuka.

Pili, kukimbilia kutoa hukumu

Mfanyakazi anakuja ofisini kwako akilalamika kwamba mwenzake amemtukana. Kabla hata hujamsikiliza upande wa pili, unaamua kumwita mtuhumiwa na kumkaripia.

Huenda aliyelalamika ndiye aliyeanzisha ugomvi. Huenda pia kuna historia ya kutokuelewana ambayo huifahamu.

Kiongozi si hakimu anayepaswa kutoa hukumu kutokana na simulizi ya mtu mmoja. Anahitaji kuchunguza ukweli, kusikiliza pande zote na kufanya uamuzi wa haki.

Tatu, kusikiliza kwa ajili ya kujibu, si kuelewa

Umewahi kukutana na bosi ambaye mfanyakazi anapoanza kueleza tatizo, tayari anaandaa jibu? Kiongozi wa aina hii hukatiza mazungumzo, hudharau maelezo au huwasikiliza zaidi wale wanaozungumza kwa sauti kubwa.

Lakini kusikiliza si kusubiri zamu yako ya kuzungumza. Ni kutafuta kuelewa kilichotokea, sababu zake na namna wahusika walivyoathirika.

Nne, kutafuta mkosaji badala ya chanzo cha tatizo

Wafanyakazi wawili wanagombania jukumu fulani. Badala ya kuchunguza namna kazi zilivyogawanywa, unaanza kutafuta nani mwenye tabia mbaya.

Baadaye unagundua kwamba wote walipewa maagizo yanayokinzana na wakuu tofauti. Kumwadhibu mmoja hakutatatua tatizo. Chanzo chake ni mfumo mbovu wa mawasiliano na mgawanyo wa majukumu.

Tano, kutumia hasira na lugha ya kushambulia

“Wewe huwa hufanyi kazi vizuri!” au “Siku zote unaleta matatizo!” Kauli hizi zinaweza kuonekana kama ukali wa kiuongozi, lakini mara nyingi humfanya mfanyakazi ajitetee badala ya kutafakari kosa lake.

Badala ya kumshambulia mtu, eleza kitendo maalumu, athari zake na marekebisho yanayohitajika.

Sita, kutaka kushinda mabishano

Kwa baadhi ya viongozi, kukubali hoja ya mfanyakazi ni sawa na kushindwa. Hivyo, hata wanapogundua wamekosea, huendelea kutetea msimamo wao ili kulinda hadhi.

Lakini mgogoro si mashindano ya kutafuta mshindi. Unaweza kushinda mabishano na kupoteza uaminifu wa timu nzima.


Saba, kukataa kutambua mchango wako katika mgogoro

Si kila mgogoro unaanzia kwa wafanyakazi. Wakati mwingine tatizo ni kiongozi mwenyewe. Anaweza kuwa anapendelea baadhi ya watu, anatoa maagizo yanayokinzana au anabadili maamuzi bila kutoa maelezo.

Kiongozi anayekataa kujitathmini anaweza kutumia muda mwingi kutatua migogoro ambayo yeye mwenyewe anaichochea.

Nane, kushughulikia migogoro yote kwa namna moja

Wafanyakazi wawili wametofautiana kuhusu mbinu ya kutekeleza mradi. Mahali pengine, mfanyakazi analalami-



MAKALA MALEZI

NA JUNAYNAT ALLY DAMA

0789 201 383

Panga hivi safari ya likizo ya familia

Mwaka unakaribia kumalizika. Watoto wanajiandaa kufunga shule, wazazi nao wanaanza kufikiria namna ya kutumia likizo za mwisho wa mwaka. Kwa baadhi ya familia, huu ni wakati wa kusafiri kwenda kuwatembelea ndugu, kutalii au kupumzika katika mazingira tofauti na yale waliyozoea.

Lakini safari nzuri haihitaji fedha nyingi pekee. Inahitaji maandalizi, bajeti inayozingatia uwezo wa familia, usalama na shughuli zinazoendana na maadili ya Kiislamu.

Kusafiri kuna faida nyingi. Kunawapa watoto nafasi ya kuona mazingira mapya, kujifunza tamaduni mbalimbali na kuongeza maarifa nje ya darasa. Pia kunasaidia familia kuwa pamoja, kuimarisha mahusiano na kupumzisha akili baada ya miezi mingi ya kazi na masomo.

Qur'an inatuhimiza kutembea duniani na kutafakari uumbaji wa Allah [Qur'an, 29:20]. Hivyo, safari ya mapumziko inaweza pia kuwa fursa ya kujifunza, kushukuru neema za Allah na kuimarisha uhusiano wa kifamilia.

Hata hivyo, likizo za mwaka huu zinahitaji tahadhari zaidi kutokana na matarajio ya mvua zinazohusishwa na El Niño.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetahadharisha kuhusu uwezekano wa mvua nyingi katika maeneo mbalimbali nchini kati ya Novemba na Januari, hali inayoweza kusababisha mafuriko na kuathiri miundombinu ya usafiri.

Kwa hiyo, familia zinazopanga kusafiri zinapaswa kuzingatia mambo yafuatayo.

Mosi, chagua mahali panapofaa familia yako.

Si lazima kwenda nje ya nchi au kwenye hoteli ya gharama kubwa ili kufurahia likizo. Tanzania ina maeneo mengi ya kuvutia, yakiwemo fukwe, hifadhi za wanyamapori, maeneo ya kihistoria na mandhari nzuri za asili.

Chagua eneo kwa kuzingatia umri wa watoto, maslahi yao, usalama, uwezo wa kifedha na upatikanaji wa huduma muhimu. Washirikishe watoto katika kuchagua maeneo ya kutembelea ili wajisikie sehemu ya maandalizi.

Pili, zingatia misingi ya Kiislamu

Kabla ya kufanya malipo ya malazi, chunguza upatikanaji wa chakula cha halali, sehemu za kuswali na shughuli za burudani zinazofaa familia ya Kiislamu.

Kama mnapanga kwenda ufukweni au kuogelea, angalia maeneo yenye faragha na mazingira yanayowezesha kuzingatia stara.

Panga shughuli zako bila kuathiri Swala tano. Watoto nao wafundishwe kuwa mapumziko si sababu ya kusahau ibada.

Tatu, andaa bajeti na epuka matumizi ya kujionyesha

Likizo haipaswi kuiacha familia katika madeni au matatizo ya kifedha. Kokotoa gharama za usafiri, malazi, chakula, viingilio na matumizi mengine. Tenga pia fedha kwa dharura.

Badala ya hoteli ghali, unaweza kuchagua nyumba za wageni au malazi yenye sehemu ya kupikia ili kupunguza gharama za chakula.

Ni bora safari ya siku mbili unayoweza kuimudu kuliko safari ya wiki moja inayohatarisha mahitaji muhimu ya familia.

Kabla ya kuondoka, fuatilia taarifa za TMA kuhusu hali ya hewa katika eneo unaloelekea na barabara mtakazotumia.

Epuka kupanga safari kwenye maeneo yenye hatari kubwa ya mafuriko, vivuko visivyo salama au barabara zinazoweza kukatika.

Ikiwa unasafiri kwa gari, hakikisha lina hali nzuri. Usijaribu kuvuka barabara iliyofunikwa na maji ambayo kina chake hukijui. Kuwa tayari kubadilisha ratiba au kuahirisha safari ikiwa hali ya hewa si salama.

Tano, panga ratiba rafiki kwa watoto

Usijaze kila siku shughuli nyingi zinazowachosha watoto. Chagua shughuli moja au mbili muhimu kwa siku, huku ukiacha muda wa kupumzika, kula na kuswali.

Watoto wadogo wanahitaji muda wa kulala na kucheza. Safari inayowachosha kupita kiasi inaweza kugeuka kuwa chanzo cha usumbufu badala ya furaha.

Sita, andaa mahitaji muhimu mapema

Beba dawa za kawaida zinazofaa familia, vifaa vya huduma ya kwanza, maji salama, vitafunwa vya halali na nguo zinazoendana na hali ya hewa.

Usisahau mavazi ya Swala, vifaa vya watoto wadogo na nyaraka muhimu za safari.

Pia hakikisha watoto wanajua namna ya kuwasiliana na wazazi iwapo watatenganа katika maeneo yenye watu wengi.

Saba, safari iwe darasa la maisha.

Watoto wanapotembelea maeneo mapya, waeleze historia, utamaduni na umuhimu wa kuhifadhi mazingira. Wafundishe kuheshimu wenyeji, kutotupa taka ovyo na kuthamini tofauti za maisha.

Muhimu zaidi, tumieni muda huo kuzungumza na watoto, kuwasikiliza na kujenga kumbukumbu nzuri za kifamilia.

Hatimaye, likizo yenye mafanikio si ile iliyogharimu fedha nyingi au iliyofanyika mbali zaidi.

Likizo bora ni ile inayorudisha familia nyumbani ikiwa salama, imepumzika, imejifunza mambo mapya na imeimarisha upendo bila kuvunja misingi ya dini.

MAKALA ELIMU

Na Samrath Msuya

0789 201 383

Ipi motisha bora: zawadi kwa matokeo au juhudi

Mzazi mmoja anasema: "Ukipata nafasi ya kwanza darasani, nitakununulia baiskeli!" Mwingine anasema: "Ukisoma kitabu kimoja kila wiki na kunieleza ulichojifunza, nitakupa zawadi."

Wazazi hawa wawili wana lengo moja: Kuwahamasisha watoto wao kusoma kwa bidii na kufanya vizuri shuleni. Hata hivyo, wanatumia njia mbili tofauti.

Mzazi wa kwanza anaahidi zawadi kwa matokeo ya mwisho, yaani ufaulu. Wa pili anatoa zawadi kwa juhudi na hatua ndogo za kujifunza, akiamini kwamba hatimaye zitaongeza ufaulu.

Swali ni hili: Njia ipi ina nafasi kubwa ya kumsaidia mtoto kufanya vizuri shuleni? Na je, zawadi zinaweza kumfanya mtoto apende elimu au zikamzoesha kusoma kwa kutegemea malipo?

Tuchunguze faida na mapungufu ya kila njia.

Zawadi kwa matokeo mazuri

Njia hii imezoeleka katika familia nyingi. Mtoto anaahidiwa fedha, simu, baiskeli au safari akipata alama fulani au kushika nafasi nzuri darasani.

Faida yake ya kwanza ni kumpa mtoto lengo linaloeleweka. Anajua anachotakiwa kufikia na zawadi inayomsubiri.

Pia, zawadi kubwa inaweza kumshawishi mtoto kuongeza juhudi, hasa kama anaamini ana uwezo wa kufikia lengo hilo. Hata hivyo, njia hii ina udhaifu muhimu.

Tatizo la kwanza ni kwamba mtoto anaweza kujua anachotaka kufikia, lakini asijue namna ya kukifikia.

Kwa mfano, mtoto anayepata alama 40 katika hesabu anaweza kutamani sana kupata 90 ili apewe baiskeli. Lakini kutamani ufaulu si sawa na kujua namna ya kuuboresha.

Anaweza kuhitaji maelezo ya ziada, mazoezi au msaada wa mwalimu. Zawadi peke yake haimfundishi njia hizo.

Tatizo la pili ni kwamba matokeo hayaamuliwi na juhudi pekee. Uwezo wa awali, ubora wa ufundishaji, mazingira ya kujifunza na ugumu wa mtihani pia vinaweza kuchangia.

Mtoto anaweza kujitahidi sana, akapanda kutoka alama 40 hadi 65, lakini asipate zawadi kwa sababu hakufikia 90.

Badala ya kufurahia maendeleo yake, anaweza kujiona ameshindwa.

Tatizo la tatu ni hatari ya kuthamini alama kuliko maarifa. Mtoto anaweza kukariri majibu kwa ajili ya mtihani, kuchagua masomo rahisi au hata kushawishika kudanganya ili kupata zawadi.

Kwa hiyo, njia hii inaweza kuongeza shauku ya kufaulu bila kuhakikisha kwamba mtoto anajifunza vizuri.

Zawadi kwa juhudi za kujifunza

Njia ya pili inaangalia mambo anayofanya mtoto kila siku badala ya kusubiri matokeo ya mwisho.

Mzazi anaweza kutoa zawadi ndogo mtoto anapomaliza kusoma kitabu, kufanya mazoezi ya hesabu au kukamilisha kazi za nyumbani.

Faida yake kubwa ni kwamba inahamasisha vitendo vinavyoweza kumfikisha mtoto kwenye ufaulu.

Badala ya kumwambia tu "Pata alama 90," mzazi anamwelekeza kwenye hatua zinazoweza kumsaidia kufikia alama hizo.

Pia, mtoto ana nafasi ya kuona mafanikio madogo bila kusubiri mwisho wa muhula.

Mtoto aliyekuwa hasomi kabisa anaweza kuanza kusoma kurasa chache kila siku. Baadaye akazidisha muda na idadi ya vitabu. Hatua hizo zinaweza kujenga mazoea mazuri ya kujifunza.

Faida nyingine ni kwamba mtoto anapewa motisha kwa mambo yaliyo ndani ya uwezo wake.

Hata hivyo, njia hii nayo ina mapungufu.

Mtoto anaweza kusoma kurasa nyingi bila kuelewa alichosoma, au kukamilisha kazi kwa haraka ili kupata zawadi.


Kwa hiyo, si kila juhudi inaongeza maarifa. Mzazi anapaswa kuangalia ubora wa kujifunza, si idadi ya kazi zilizokamilishwa pekee.

Pia kuna hatari ya mtoto kuzoea kutaka zawadi kwa kila shughuli. Badala ya kujifunza kwa hamu yake mwenyewe, anaweza kuanza kuuliza atalipwa nini.

Kwa hiyo, njia ipi bora?

Kwa ujumla, zawadi kwa hatua za kujifunza zina faida zaidi, hasa kwa watoto wanaohitaji kujenga mazoea ya kusoma.

Sababu ni rahisi: Ufaulu ni matokeo, lakini kujifunza ni mchakato. Mtoto ana nafasi kubwa ya kuboresha matokeo anapojenga tabia zinazochangia ufaulu.



Hata hivyo, njia bora si kutoa zawadi kwa kila ukurasa anaosoma. Ni kutambua juhudi zenye maana, kupima uelewa wake na kumsaidia kuona maendeleo anayopiga.

Zawadi pia zinaweza kupunguzwa taratibu kadiri mtoto anavyoanza kufurahia kujifunza.

Mzazi anaweza kuendelea kusherehekea matokeo mazuri, lakini asifanye nafasi ya kwanza kuwa kipimo pekee cha mafanikio.

Hatimaye, zawadi bora si inayomfanya mtoto asome leo ili apate baiskeli kesho, bali inayomsaidia kujenga mazoea ya kujifunza hata wakati hakuna zawadi inayomsubiri.

٣٠ جُمَادَى الأُولَى ١٤٤٨ هـ

TUJIFUNZE

AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

Na Junaynat Ally Dama

Uandishi wa habari kwa msaada wa AI

SEHEMU YA 10

Hatua 7 za kujiandaa kutumia AI chumba cha habari

Mpaka sasa tumeangalia namna mwandishi mmoja mmoja anavyoweza kutumia akili bandia (AI) kutafuta na kuendeleza wazo, kukusanya taarifa, kuchambua nyaraka, kuandika, kuhariri na kuandaa habari kwa majukwaa mbalimbali.

Lakini matumizi salama ya AI hayawezi kubaki kuwa suala la mwandishi mmoja mmoja. Chumba cha habari kinahitaji kujiuliza: Tunataka kuitumia kwa kazi gani, kwa mipaka gani na nani atawajibika inapokosea?

Kujiandaa vizuri hakumaanishi kununua programu nyingi za AI bali kuelewa teknolojia, mahitaji ya chumba cha habari na wajibu wa uandishi wa habari.

Hatua 1: Elewa AI ni nini na si nini

Chumba cha habari hakiwezi kupanga matumizi ya teknolojia ambayo watu wake hawaielewi. Waandishi na wahariri wanahitaji kuelewa kwa kiwango cha msingi AI inaweza kufanya nini, inapungukiwa wapi na kwa nini majibu yake yanahitaji kuhakikiwa.

Tusione AI kama kama suluhisho la kila tatizo wala tusiikatae kabisa kwa hofu itachukua nafasi zetu. Badala yake, AI iwe zana ya kuongeza uwezo wa watu, lakini pia isichukue nafasi ya uamuzi wa kiuhariri, maadili, uwajibikaji na uhusiano wa mwandishi na vyanzo.

Hatua 2: Tambua inaweza kusaidia wapi

Chumba cha habari kiangalie kazi zake za kila siku. Ni maeneo gani yanatumia muda mwingi? Ni kazi zipi zinajirudia? Ni wapi waandishi wanahitaji msaada zaidi?



Huenda jibu likawa kunukuu mahojiano, kupitia nyaraka nyingi, kupanga takwimu, kutengeneza muhtasari, kutafsiri au kuandaa habari kwa majukwaa mbalimbali.

AI isiingizwe kila mahali kwa sababu tu ipo bali itumike kuongeza uwezo wetu bila kushusha ubora wa habari.

Hatua 3: Anza na tatizo, si teknolojia

Taasisi inaona programu mpya ya AI na kujiuliza, "Tutaitumiaje?" Bora kuanza upande mwingine: "Tunataka kutatua tatizo gani?"

Kama chumba cha habari kinatumia saa nyingi kunukuu mahojiano, teknolojia itumike. Kama waandishi wanapitia mamia ya kurasa za ripoti, AI isaidie katika uchambuzi wa awali. Kama changamoto ni kuandaa habari kwa majukwaa mengi, hapo pia inaweza kuwa na nafasi.

Teknolojia inapaswa kufuata mahitaji ya kazi, si kazi kulazimishwa kufuata teknolojia.

Hatua 4: Angalia namna kazi za watu zitakavyobadilika

AI inaweza kupunguza baadhi ya kazi zinazojirudia, lakini inaweza pia kubadilisha ujuzi unaohitajika katika chumba cha habari.

Mwandishi anayepata nakala ya mahojiano anaweza kutumia AI kuipeleka katika maandishi. Hata hivyo, lazima ahakiki. Mhariri anayetumia AI kupitia rasimu bado anahitaji jicho la lugha, ukweli na haki.

Kwa hiyo, Chumba cha habari kinahitaji kuwekeza katika mafunzo. Waandishi wajue si tu namna ya kutumia AI, bali pia namna ya kuhoji majibu yake, kutambua makosa na kujua wakati gani wasiitumie.

Hatua 5: Tambua vikwazo mapema

Si kila chumba cha habari kina mazingira sawa. Gharama za teknolojia zinaweza kuwa changamoto. Wengine wanaweza kukosa vifaa, intaneti ya uhakika au watu wenye ujuzi wa kutosha.

Kuna pia hofu za kupoteza ajira, kutokuamini teknolojia na kutokuwa na mkakati wa pamoja, hali inayoweza kuongeza hatari badala ya kuongeza ufanisi.

Kwa hiyo, chumba cha habari kinahitaji kujua vikwazo vyake kabla ya kuamua matumizi yake. Si lazima kila taasisi ifanye kila kinachofanywa na chumba cha habari kikubwa chenye rasilimali nyingi.

Hatua 6: Weka kanuni kabla tatizo halijatokea

Chumba cha habari kinachotumia AI kinahitaji muongozo unaoeleweka. Je, mwandishi anaweza kuingiza mahojiano ya chanzo cha siri kwenye AI? Je, picha zinazotengenezwa na AI zinaweza kutumika? Zikitumika, msomaji ataambiwa? Je, AI inaweza kuandika habari nzima? Ni nani anayehakiki matokeo yake?

Maswali hayo yasiachwe mpaka kosa litokee. Sera nzuri iwe muongozo unaowaambia waandishi kile kinachoruhusiwa, kile kinachohitaji tahadhari na kile ambacho hakikubaliki.

Hatua 7: Jaribu, jifunze na shirikisha watu tofauti

Chumba cha habari hakihitaji kuanza kwa kubadilisha mfumo mzima wa kazi. Anzeni na jaribio dogo katika eneo moja, kuona manufaa na matatizo, kisha kujifunza kabla ya kupanua matumizi.

Ni vizuri pia maamuzi kuhusu AI yasiwe ya wahariri au wataalamu wa teknolojia pekee. Waandishi, wahariri, watu wa data, wabunifu na wataalamu wengine wanaweza kuona hatari na fursa tofauti.

Kadiri matumizi yanavyoongezeka, rudini katika kanuni zenu. Teknolojia inabadilika kwa kasi, hivyo sera iliyofaa leo inaweza kuhitaji marekebisho kesho.

٣٠ جُمَادَى الأُولَى ١٤٤٨ هـ

MAKALA YA AFYA

Na Junaynat Ally Dama



Dalili unahitaji kumuona mtaalamu wa afya ya akili

Kila mmoja wetu hupitia vipindi vya huzuni, msongo wa mawazo, wasiwasi au kukata tamaa. Hali hizi ni sehemu ya maisha. Lakini swali muhimu ni hili: Unajuaje kwamba unachopitia si changamoto ya kawaida, bali tatizo linalohitaji msaada wa mtaalamu wa afya ya akili?

Wataalamu wanaeleza kuwa watu wengi huchelewa kutafuta msaada kwa sababu hudhani matatizo yao yatakwisha yenyewe. Wengine huamini kwamba kwenda kupata ushauri wa kisaikolojia ni kwa watu wenye magonjwa makubwa ya akili pekee.

Hata hivyo, wanasaikolojia wanaeleza kwamba kutambua mapema mabadiliko ya kihisia, kitabia na kiutendaji kunaweza kumsaidia mtu kutafuta msaada kabla hali haijawa mbaya.

Kwa kuzingatia maelezo ya wataalamu mbalimbali, zifuatazo ni dalili 10 zinazopaswa kukufanya ufikirie kupata msaada wa kitaalamu.

Mosi, huzuni au wasiwasi unaodumu muda mrefu.

Ni kawaida kuhuzunika baada ya kupoteza kazi, kufiwa au kukumbwa na changamoto nyingine. Hata hivyo, huzuni, hofu au kukata tamaa vinapoendelea bila nafuu, hasa kwa wiki mbili au zaidi, vinaweza kuashiria tatizo linalohitaji uchunguzi.

Pili, kujitenga na watu.

Mtu aliyekuwa akifurahia kukutana na marafiki, ndugu au kushiriki shughuli za kijamii anaweza kuanza kujitenga. Kutamani kuwa peke yako si tatizo lenyewe, lakini kujitenga kupita kiasi na kuacha mahusiano muhimu kunaweza kuwa ishara ya changamoto za afya ya akili.

Tatu, kupoteza hamu ya mambo uliyokuwa ukiyapenda.

Huenda zamani ulipenda michezo, kusoma, kusafiri au kukutana na marafiki. Sasa hakuna kinachokufurahisha. Kupoteza uwezo wa kufurahia shughuli za kawaida ni mojawapo ya dalili zinazoweza kuhusishwa na sonona, kitaalamu depression.

Nne, mabadiliko makubwa ya usingizi.

Kukosa usingizi, kuamka mara kwa mara au kulala kupita kiasi kunaweza kuhusishwa na matatizo ya kihisia. Hata hivyo, mabadiliko hayo yanaweza pia kutokana na magonjwa ya mwili, dawa au mazingira ya maisha.

Tano, kushindwa kutekeleza majukumu ya kawaida.

Unapoanza kushindwa kufanya kazi, kusoma, kutunza familia au kukamilisha majukumu ambayo hapo awali hayakukusumbua, ni muhimu kuchunguza sababu. Kushuka kwa uwezo wa kufanya shughuli za kila siku kunaweza kuonyesha kwamba changamoto imeanza kuathiri maisha yako.

Sita, matatizo ya kumbukumbu na umakini.

Kusahau mara kwa mara, kushindwa kufanya maamuzi rahisi au kupoteza umakini kunaweza kuhusishwa na msongo wa mawazo, wasiwasi au sonona. Hata hivyo, dalili hizo peke yake hazithibitishi ugonjwa wa akili.

Saba, uchovu usioelezeka.

Mtu anaweza kujisikia amechoka muda wote, hata baada ya kupumzika. Wakati mwingine uchovu huu huambatana na kupoteza ari ya kufanya shughuli za kawaida. Ni muhimu pia kuchunguza uwezekano wa matatizo mengine ya kiafya.

Nane, mabadiliko makubwa ya hamu ya kula na kujitunza.

Kupoteza hamu ya chakula, kula kupita kiasi au kushindwa kuzingatia usafi binafsi kunaweza kuonyesha kwamba mtu anapitia changamoto kubwa. Mabadiliko yanayoendelea yanahitaji kuangaliwa kwa makini.

Tisa, kujilaumu kupita kiasi na kushindwa kudhibiti hisia.

Kujiona hufai, kujilaumu kila wakati, kukasirika kupita kiasi au kushindwa kudhibiti wasiwasi kunaweza kuathiri mahusiano na ustawi wa mtu. Hisia hizi zinapoendelea au kuongezeka, ushauri wa kitaalamu unaweza kusaidia.

Kumi, mawazo ya kujidhuru au kujiua.

Hii ni dalili inayohitaji msaada wa haraka. Mtu anayefikiria kujiumiza au kujiua hapaswi kusubiri hali ijirekebishe yenyewe. Anahitaji kuzungumza na mtu anayeaminika na kupata msaada wa dharura kutoka kwa wataalamu wa afya.

Ni wakati gani wa kutafuta msaada?

Kwa mujibu wa Taasisi ya Taifa ya Afya ya Akili ya Marekani, dalili zinazodumu, zinazoongezeka au zinazoathiri utendaji wa kila siku zinapaswa kuchunguzwa. Si lazima mtu awe amefikia hatua ya kushindwa kabisa kuendesha maisha ndipo atafute msaada.

Muhimu zaidi, dalili hizi si uthibitisho wa ugonjwa. Uchunguzi wa kitaalamu ndiyo unaoweza kusaidia kubaini tatizo na aina ya msaada unaohitajika.

Kumbuka, kama tunavyotafuta matibabu tunapougua mwili, ndivyo tunavyopaswa kuthamini afya ya akili. Kutafuta msaada mapema si udhaifu, bali ni hatua muhimu ya kujilinda na kuboresha maisha.

MAKALA SAIKOLOJIA

Na Ukhti Fatima SS

0789 201 383

Wazazi tunapotesa watoto kihisa bila kujua

Mtoto amerudi kutoka shuleni akiwa na furaha. Amepata alama 80 kwenye mtihani na anakimbilia kumwonyesha mama yake karatasi ya matokeo. Badala ya pongezi, mama anamuuliza: "Mbona hukupata 100? Mwenzako alipata ngapi?"

Furaha ya mtoto inapotea ghafla. Ananyamaza na kuondoka. Mama anaendelea na shughuli zake, akiamini amemhamasisha mwanawe kusoma kwa bidii. Lakini huenda amemuumiza kisaikolojia bila kujua.

Hali kama hii hutokea katika familia nyingi. Wazazi wanaweza kuwapenda watoto wao, kuwapatia mahitaji muhimu na kujitahidi kuwajengea maisha mazuri, lakini wakati huohuo wakawaumiza kihisia kupitia maneno, vitendo au mbinu za malezi.

Wataalamu wa saikolojia wanaeleza kwamba unyanyasaji wa watoto si kupigwa, kuchomwa au kujeruhiwa pekee. Unaweza pia kujitokeza kupitia kudhalilishwa, kutishiwa, kupuuzwa au kunyimwa upendo na mahitaji ya kihisia.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linaonya kwamba unyanyasaji wa utotoni unaweza kuathiri afya ya akili, maendeleo ya ubongo, uwezo wa kujifunza na mahusiano ya mtu hata anapokuwa mtu mzima.

Lakini wazazi wanawezaje kuwaumiza watoto bila kutambua? Zipo tabia mbalimbali zinazopaswa kutafakariwa.

Mosi, kumlinganisha

"Mbona huwezi kuwa kama dada yako?" "Mwenzako anaongoza darasani, wewe una matatizo gani?"

Mzazi anaweza kudhani anahamasisha ushindani, lakini kumlinganisha mtoto mara kwa mara kunaweza kumjengea hisia kwamba hana thamani au hapendwi kama wengine.

Watoto hutofautiana kwa uwezo, vipaji na kasi ya kujifunza. Ni muhimu kupima maendeleo ya mtoto kwa kuzingatia uwezo na juhudi zake.

Pili, maneno yanayodhalilisha.

"Mjinga wewe!" "Huna akili!" "Hutakuja kufanikiwa!" Maneno haya yanaweza kutamkwa wakati wa hasira na kusahaulika haraka na mzazi. Lakini mtoto anaweza kuyaweka moyoni kwa muda mrefu.

Mtoto anaposikia mara kwa mara kwamba hafai, anaweza kuanza kuamini hivyo. Hali hii inaweza kudhoofisha kujiamini na namna anavyojithamini.

Tatu, kupuuza hisia za mtoto

Mtoto analia kwa sababu amepoteza kitu anachokipenda. Mzazi anamwambia: "Nyamaza! Unalia vitu vya kipuuzi!" Kwa mtu mzima, jambo hilo linaweza kuonekana dogo. Lakini kwa mtoto linaweza kuwa muhimu sana.

Kupuuza hisia zake mara kwa mara kunaweza kumfundisha kwamba huzuni, hofu au maumivu yake hayana umuhimu.

Nne, malezi ya vitisho

"Nitakufukuza nyumbani!" "Nitakuacha hapa peke yako!" "Ukifanya hivyo tena, hutakuwa mwanangu!"

Mzazi anaweza kutamka maneno haya ili mtoto atii. Lakini vitisho vya kuachwa au kukataliwa vinaweza kuathiri hisia za usalama ambazo mtoto anahitaji. Mtoto anahitaji mipaka na nidhamu, lakini pia uhakika kwamba anapendwa hata anapokosea.

Tano, kumnyimwa upendo kama adhabu

Baadhi ya wazazi huacha kuzungumza na watoto wao, kuwajibu au kuwaonyesha mapenzi wanapokosea. Ingawa mzazi anaweza kuhitaji muda wa kutulia, kumtenga mtoto kihisia kama adhabu kunaweza kumfanya ajione amekataliwa.

Ni muhimu kutofautisha kukemea tabia mbaya na kumfanya mtoto aamini kwamba yeye mwenyewe ni mbaya.

Sita, matarajio tofauti na umri wake.

Mtoto mdogo anatarajiwa kukaa kimya muda mrefu, kutokosea au kutekeleza majukumu yanayozidi uwezo wake. Anaposhindwa, anaadhibiwa.

Wataalamu wanashauri wazazi kuelewa hatua za ukuaji wa watoto. Si kila tabia inayoudhi ni ukaidi; wakati mwingine ni sehemu ya kawaida ya ukuaji.

Saba, mazingira ya migogoro

Wazazi wanapogombana kila mara, kutukanana au kutishiana mbele ya watoto, wanaweza kuwaathiri hata kama hawawagusi.

Mtoto anaweza kuanza kuishi kwa hofu, wasiwasi au kujiona mwenye hatia kwa matatizo ya wazazi wake.



Utajuaje mtoto ameathirika?

Mabadiliko ya tabia yanaweza kutoa tahadhari. Mtoto anaweza kujitenga, kuwa mkali, kuogopa makosa kupita kiasi, kupata matatizo ya usingizi au kushuka kitaaluma.

Wengine wanaweza kurudia tabia za umri mdogo, kama kukojoa kitandani. Hata hivyo, dalili hizi hazithibitishi unyanyasaji. Zinaweza kuwa na sababu nyingine zinazohitaji kuchunguzwa.